SUPA JACKPOT
TZS.1,072,549,524
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

NHC

**Thamani** NHC yapanda, sasa yafikia tril. 5/-

UKURASA 4




UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Februari 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581209
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Samia awaibua Kitwanga, LHCR

• **Kuhusu** madudu Polisi, DPP na Takukuru, akomalia sheria kikwazo utoaji haki... *Endelea ukurasa 2*



Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga

**"Tatizo kubwa linalochangia ni uadilifu hafifu wa baadhi ya watendaji, pia sheria zilizopo za uwajibishaji hazina meno kuwachukulia hatua.**



Charles Kitwanga

**"Tume hiyo imulike zaidi na kwenye wizara zote ili kuhakikisha uadilifu unatawala na kila kiongozi anayepewa dhamana anaitekeleza kwa weledi, haki na uadilifu.**



Dk. George Kahangwa

**"Watanzania hatupendi kuona taasisi zenye madudu, wala viongozi wasio waadilifu. Tunataka taasisi na viongozi walioimarika kila eneo.**

## Mfumo matokeo NECTA wazua jambo bungeni

UKURASA 3




Zaidi ya wafanyakazi 60 wa kampuni ya usafi ya Green Waste, wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali, walipofanya maandamano hadi katika ofisi za kampuni hiyo, jijini Mwanza jana, wakidai kulipwa malimbikizo ya mishahara yao ya miezi sita yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 51. **PICHA: VITUS AUDAX**

# ACT- Wazalendo 'yafukua makaburi' waathirika wa mabomu ya Mbagala

UKURASA 3

**MICHEZO** SPORTPESA YAIWAKIA YANGA SC UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Jaji Mkuu, Ibrahim Hamis Juma (wa pili kulia), baada ya Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania kwenye viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma jana. Kulia ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia awaibua Kitwanga, LHRC

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kubainisha madudu yaliyomo ndani ya taasisi nyeti za serikali, amewaibua wadau ambao wametoa maoni huku wakimpongeza kwa hatua aliyochukua ya kuunda tume ya kuzichunguza.

Licha ya kupongeza kwa uamuzi wa kuunda tume, wadau hao wamesema anapaswa pia kuzifumua na kuzisuka upya ili kuleta ufanisi katika utendaji.

Miongoni mwa taasisi ambazo zilitajwa na Rais Samia ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Jeshi la Polisi na Tume ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Rais Samia alisema ndani ya taasisi hizo kumekuwa na mmonyoko wa maadili, upendeleo katika upandishaji vyeo, kuwabambika watu kesi zikiwamo za uhujumu na dawa za kulevya na mambo mengine ambayo yamesababisha jamii kukosa imani nazo.

Wakizungumza na Nipashe juu ya uamuzi wa Rais Samia, baadhi yao walimpongeza huku wengine wakitoa ushauri kwamba tume hiyo iende hadi katika wizara mbalimbali.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Charles Kitwanga, alisema hatua iliyochukuliwa na kiongozi huyo wa nchi ni nzuri na kushauri tume hiyo imulike zaidi na kwenye wizara zote ili kuhakikisha kwamba uadilifu unatawala na kila kiongozi anayepewa dhamana anaitekeleza ipasavyo kwa weledi, haki na uadilifu.

Pia alishauri kwamba watakaobainika kuchangia kushuka kwa weledi na kukithiri kwa 'madudu' yaliyotajwa na Rais Samia katika taasisi hizo, wachukuliwe hatua za haraka ikiwamo kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kitwanga alisema kuna tabia ya kulegea kwa uadilifu na utendaji ambayo imeanza kujionyesha kwa baadhi ya watendaji katika baadhi ya taasisi za serikali na kwamba hilo halipaswi kuachwa bali linatakiwa kushughulikiwa kwa uharaka ili lisiote mizizi na kuharibu yale mazuri yanayofanyika.

"Kwanza hawa viongozi walipo kwenye hizi taasisi wanatakiwa wamshukuru Rais kwa sababu amekuwa mstaarabu sana lakini wasichukulie ustaarabu na upole wake kutaka kumkanyaga kichwani. Nimpongeze kiongozi huyu mkuu wa nchi kwa kuliona hilo na kuunda tume ya kuchunguza suala hilo.

"Lakini asiishie kwenye hizo taasisi nyeti alizozitaja, aingie hata kwenye wizara zote huko nako kuna madudu mengi sana, tena ikibidi aongeze na kaukali kidogo maana wameanza kuchukulia kama 'busness as usual' (kufanya kazi kwa mazoea). Wameanza kulegea makazini, hiyo siyo nzuri kwetu inabidi tupambane kukomesha," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi huo lakini akasema tatizo linalochangia kuwapo na madudu hayo kwenye hizo taasisi ni kukosekana kwa uadilifu kwa baadhi ya watendaji.

"Tatizo kubwa linalochangia hali hiyo ni uadilifu hafifu wa baadhi ya watendaji, pia sheria zilizopo za uwajibishanaji hazina meno kuwachukulia hatua, hivyo mfumo mzima unatakiwa ufumuliwe. Tuna imani na tume iliyoteuliwa italeta majibu na suluhisho la muda mrefu," alisema Henga.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Dk. George Kahangwa, alisema hatua ya Rais kufikia hatua ya kutoa kauli kali kuhusu taasisi hizo tayari ana taarifa za kutosha kuhusu uwapo wa tatizo.

Alisema hivyo ni vema Rais Samia akazifumua ili kurejesha uadilifu kwenye taasisi hizo na uwajibikaji kwa viongozi wanaopewa nafasi.

"Watanzania hatupendi kuona taasisi zenye madudu, wala viongozi wasio waadilifu, tunataka taasisi na viongozi walioimarika kila eneo. Ninaami kwamba tayari Rais ana taarifa zinazojitosheleza juu ya taasisi hizo, azifumuwe na kama ikiwezekana anaweza na yeye kuwa na kauli mbiu yake ya kuwajibisha watendaji wake kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake," alisema. Dk.Kahangwa alisema taasisi zilizotajwa na Rais Samia ni nyeti na ndizo zinategemewa na nchi kwa suala la kusimamia uadilifu hivyo kama zenyewe ndizo zitakuwa kinara wa kubomoa ni hatari kwa taifa.

"Kwa mfano unapotaja polisi, TAKUKURU na DPP, hizi ni taasisi hatutarajii kuona zinatajwa kuwa na madudu, kukosa uadilifu au kutajwa tena kwenye vitendo vya rushwa. Hii ni hatari na nafikiri ifike mahali hata wale wanaoteuliwa kwenye hizi waangaliwe viwango vyao vya uadilifu na ikibidi ziwe zinapimwa kila mwaka," alisisitiza.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**CAROLINE NOELA GICHURU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUBARU FORESTER yenye usajili namba **T638 DGW,** CHASSIS NAMBA: **SG5083493** na ENGINE NAMBA: **C408235.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/45144/2023**

21725902



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 254 YA MWAKA 2022**

**NADO MACHELA ........................................................MDAI**

**VERSUS**

**MNADI MKWAI MPILIMU ......................................MDAIWA**

**KWA:**
**MNADI MKWAI MPILIMU**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 17.02. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO**: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 ya mwezi wa JANUARI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA


## ... Akomalia sheria kikwazo utoaji haki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amezidi kuwasha moto wa kutaka sheria zinazokwamisha utoaji haki kufanyiwa marekebisho.

Katika kutaka kutekelezwa jambo hilo, ameitaka Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha na Mipango, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushirikiana ili kuzifanyia marekebisho sheria zote zenye mizunguko zinazochelewesha mashauri yanayohusu masuala ya fedha na kodi.

Dk. Samia alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipokuwa akihutubia wananchi na viongozi mbalimbali kwenye maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria nchini.

"Ni kweli kwamba mashtaka mengi hasa yanayohusu uchumi kama fedha na kodi yanapitia hatua nyingi mpaka kukamilika kwake, hivyo nitoe wito kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na watu wote wanaohusika kushirikiana na kuzifanyia marekebisho sheria zote zenye mizunguko inayochelewesha kesi na upatikanaji wa haki mapema.

"Wenyewe mnasema kucheleweshwa kwa kesi ni kuchelewesha haki si ndiyo? Kwa kizungu mimi nimeitafsiri kwa kiswahili nilivyoelewa," alisema Samia.

Alisema kutokana na kesi nyingi kuchukua muda mrefu mahakamani, ni vyema usuluhishi ukapewa kipaumbele kutokana na faida zake ikiwamo kupunguza gharama na muda, hivyo wananchi kupata haki zao mapema na kuondoa malalamiko.

Pia aliwataka majaji, Mahakimu na wadau wote katika sekta ya sheria kupitia upya taratibu ambazo mashauri hupitia ili kuyafupisha kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa haki.

"Nchi yetu imejengwa kwa misingi inayozingatia haki inayodumisha amani tuliyo nayo. Amani hutoweka endapo tu migogoro inafikishwa mahakamani lakini haitatuliwi kwa haraka. Ukiangalia panapotokea uvunjifu wa amani mara nyingi kunakuwa haki imepotezwa kwa hiyo tujitahidi sana haki ipatikane mapema ili amani iwapo nchini," alisema.

Kadhalika, alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wananchi kwa kupitia upya mifumo iliyopo ya utoaji haki nchini. "Kama mnavyojua au mlivyoona jana (juzi) nilizindua tume ya kuangalia mienendo ya taasisi za haki jinai inayoongozwa na Mwenyekiti wake Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania, Othman Chande na makamu wake Balozi Ombeni Sefue, itafanya kazi yake kwa muda wa miezi minne. Itaangalia mifumo, maslahi ya watumishi na uhaba wa watumishi" alisema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema iko haja utatuzi wa kesi za migogoro kutumia njia ya usuluhishi badala ya mahakama ili kuokoa muda ambao umekuwa ukitumika kutolewa kwa uamuzi.

Alisema ziko baadhi ya kesi za migogoro ya kazi ambazo zingeamuliwa kwa kutumia njia ya usuluhishi kama vile Tume ya Usuluhishi na Uamuzi zingetumia muda wa siku 30, lakini kutokana na kupelekwa Mahakamani zilitolewa maamuzi baada ya miaka saba. "Hasara za kesi za migogoro kuletwa Mahakamani ni pamoja na kutumia muda mwingi, gharama za uendeshaji kesi lakini baadhi ya mali kushikiliwa hadi kesi itakapoisha hivyo wawekezaji wengi hawawezi kuvumilia kuona mitaji yao inakufa" alisema Prof. Juma

Hata hivyo, alisema Bunge lilipitisha sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali Na.1 ya mwaka 2020 iliyozifanyia marekebisho sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai sura ya 33 kwa kuongeza kifungu kipya cha 64A, kinachotamka kuwa wadaawa sasa wana hiari ya kutatua mgogoro nje ya mahakama.

## HABARI KITAIFA

# ACT Wazalendo 'yafufua makaburi' ya waathirika mabomu ya Mbagala

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kimepokea malalamiko kutoka kwa waathirika wa mabomu ya Mbagala kuhusu kutolipwa fidia huku wengine wakidai kutolipwa viwango stahiki.

Sambamba na kuibua hayo, chama hicho pia kimesema kumekuwa na madai ya baadhi ya watu waliolipwa ambao hawakuathirika na wala si wakazi wa eneo hilo. Athari za mabomu kwa wananchi zilitokea Aprili 29, 2009 kutokana na kulipuka kwa ghala la silaha katika kambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikodi 671 KJ kilichoko Mbagala.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Waziri Mkuu Kivuli wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu (pichani), alisema milipuko hiyo ilisababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa mali za wananchi zikiwamo nyumba, athari za kiafya kama magojwa ya kifua, upofu wa macho na saratani.

Semu alisema wastani wa kaya 12,000 ziliathiriwa na milipuko hiyo katika eneo la Mbagala na sehemu za jirani na kwamba kutokana na athari hizo, serikali iliamua kuangalia ustawi wa watu hao kwa kuwapatia fidia, vifuta machozi na ahadi za kushughulikia matibabu.

"ACT-Wazalendo ilifuatilia suala hilo kwa kuchambua taarifa mbalimbali kama orodha ya waathirika, malipo, risiti za malipo, kiasi cha bajeti kilichotumika na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na baadaye kutembelea baadhi ya waathirika hao.

Alibainisha kuwa baada ya kutembelea wakazi wa eneo hilo, aliona wananchi waliopatwa na ulemavu kutokana na athari za mabomu, makazi yaliyoharibiwa ambayo wamiliki wameshindwa kuyakarabati kutokana na kucheleweshewa fidia.

Pia alisema wamekabidhiwa nyaraka pamoja na risiti za malipo zinazoonyesha waathirika hao kulipwa Sh. 1,400; 2,700 na 1,900 tu. Alikumbusha kuwa katika bunge la 2022/23, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, alijibu maswali kwa niaba ya Waziri Mkuu kwa kusema waathirika walikuwa 12,647 ilihali hawakufika 10,000.

Pia alisema aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), William Lukuvi, aliwahi kusema kima cha chini walicholipwa waathirika wa mabomu ni Sh. milioni 40, huku akidai kwamba kilichofanyika ni kinyume cha maelezo hayo.

"Malalamiko mengi ya wananchi yanathibitishwa na ripoti ya CAG ya 2012/13 iliyoonyesha malipo ya fidia kwa waathirika wa mabomu ya Mbagala kiasi cha Sh. bilioni nane hayakuwa na nyaraka muhimu za kuthibitisha kama kweli malipo hayo yalifanyika kwa walengwa. Kinyume chake adhabu hiyo wanapewa wananchi kwa kunyimwa stahiki zao, vitisho na kebehi," alisema Semu.



**HATUA ZA KUCHUKUA**

Kiongozi huyo wa upinzani alitoa wito kwa Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa, kulifuatilia suala hilo na kuchukua hatua za kiuwajibikaji kwa watendaji waliolishughulikia, akidai kwamba kuna harufu ya udanganyifu, ubaguzi na uonevu.

Pia alitoa rai kwa CAG kufanya ukaguzi maalum wa fungu la Katibu Tawala wa Dar es Salaam kuona namna malipo ya fidia ya wahanga wa mabomu ya Mbagala yalivyofanyika.

Vile vile, alitoa wito kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kukamilisha uchunguzi wake ili kubaini wahusika na mchakato mzima wa utoaji malipo kwa fidia kwa watu wasiohusika na mabomu ya Mbagala, taarifa mbalimbali za ushahidi ikiwemo ya majina 1,571 yaliyolipwa mwaka 2017 na 2018 ambayo si ya wakazi wa kata 19 zilizokumbwa na kadhia hiyo, ambazo zilifikishwa ofisini kwao na waathirika waliopunjwa fidia.

"Tunawataka watumishi wa serikali kusikiliza madai ya wananchi na kutoa ufafanuzi na hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika wa kitengo cha maafa wanaotoa vitisho, kuwapisha kinyume cha sheria na kuwanyamazisha viongozi wa wahanga waliopunjwa fidia ili kuwavunja moyo wanapodai haki zao.

# Mfumo matokeo NECTA wazua jambo bungeni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

UTARATIBU mpya wa kutangaza matokeo ulioanza kutumiwa na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) mwaka jana, umehojiwa bungeni baada ya Mbunge wa Bunda Vijijini, Boniphace Getere, kutaka ufafanuzi wa serikali kutokana na kuwapo kwa minong'ono mingi.

Getere alisema kutoka Januari 28, mwaka huu, baada ya NECTA kutangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha nne, kumekuwa na minong'ono mingi kutoka kwa wananchi mpaka wabunge wenyewe na mitandao.

"Ninaomba mwongozo wako kujua baraza limekuwa likitangaza kwamba hawatatoa matokeo ya shule kutangazwa kwa shule 10 bora. Minong'ono hiyo imekuwa ikinong'ona kwamba kutotangaza 10 bora au mwisho kutaleta matatizo mengi, lakini kutadhoofisha elimu ya nchi yetu," alisema.

Getere alisema kwa kuwa serikali ipo ndani ya Bunge, kwa nini isitoe tamko au taarifa kwa wananchi wajue ni kipi bora kuhusu minong'ono hiyo inayoendelea.

Baada ya mwongozo huo, Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, alisema: "Ninafikiri hili litajibiwa vizuri na wenyewe niwape fursa kama wanalo la kujibu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia karibuni mjibu swali hilo."

Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda akitoa maelezo kuhusu uamuzi huo wa kutokutangaza shule bora kwa kutegemea matokeo ya mwisho ya mtihani alisema kuanzia miaka ya 90 ilikuwa ni kawaida baraza kutangaza shule kwa kuonyesha ipi imefanya vizuri kwenye mtihani.

"Baadaye kwenye 'Big Result Now' kukawa ni mkakati wa kupima ubora na ufanisi wa shule kwa kuangalia wanafunzi wamefaulu vipi, kwenye mtihani wa mwisho, ni kutangaza shule zipi zimefanya vizuri na zipi zimefanya vibaya, halmshauri ipi imefanya vizuri na ipi vibaya na mkoa upi umefanya vizuri na upi vibaya," alisema.

Alisema kigezo kilikuwa ni kuangalia matokeo ya mtihani wa mwisho, lakini Novemba mwaka jana baraza katika kikao chake, kiliamua kuacha kuchukua jukumu la kutangaza kwa utaratibu huo wa kutumia tu matokeo ya mwisho ya mtihani.

"Matokeo ya darasa la saba yaliyotangazwa Desemba Mosi, mwaka jana baraza halikutangaza shule 10 bora au shule 10 za mwisho, kadhalika matokeo yaliyotoka juzi ya kidato cha nne halikutangaza shule zipi bora na zipi za mwisho," alisema.

Lakini alisema takwimu zote zinazohusu kutangaza shule gani imepata A nyingi zaidi na ipi imepata kidogo na ipi ya mwisho zipo hadharani.

"Siyo siri baraza limejiondoa kwenye jukumu la kusema ni shule ipi bora, lakini mtu yeyote akitaka kuangalia ataona ni shule ipi bora, takwimu hazijafichwa mtu yeyote kuangalia shule gani ni bora," alisema na kubainisha kwamba baraza limejivua jukumu hilo kutokana na utata wa namna ya kutathmini shule bora.

"Chukua kwa mfano shule yenye wanafunzi 100 waliomaliza kidato cha nne nyingine ina wanafunzi 20, ya wanafunzi 100 wanafunzi 70 wamepata A na 30 hawakupata A, shule yenye wanafunzi 20 wote wamepata A kwa kuangaliwa wastani ni wazi shule yenye wanafunzi 20 itatangazwa kuwa ni shule bora kuliko yenye wanafunzi 100.

"Wengine watasema shule iliyoweka wanafunzi 70 wakapata A si bora zaidi kuliko shule ambayo imeleta A 20 tu, ukiacha utata huo Mheshimiwa Mwenyekiti. Aina hii ya tathmini inaweka shinikizo kwa shule ya wanafunzi 100 mfano, kuhakikisha kwamba inawaondoa wale 30 ambayo imeshaona wazi kupata A waondoke ili iweze kutangazwa shule bora kwa kupata A 70 ambayo itakuwa ni asilimia 100," alisema.






Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemia Mchechu (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya shirika hilo kwa mwaka 2021/2022 na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka 2023. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Thamani ya NHC yapanda hadi tril. 5/-

**Na Joseph Mwendapole**

MIZANIA ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), imeendelea kuimarika na thamani ya mali za shirika hilo kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa, sasa imefikia Sh. trilioni 5.04 hadi kufikia Januari 31, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemia Mchechu, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ufanisi wa shirika hilo sambamba na mafanikio ya mwaka 2021/22 na mwelekeo wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya shirika kwa mwaka 2022/23.

Alisema kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mizania hiyo imeendelea kukua mwaka hadi mwaka kwa wastani wa asilimia 12 katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2019.

"Thamani hii inahusisha vitegauchumi vya majengo na ardhi ghafi inayomilikiwa na Shirika ambayo bado haijaendelezwa ikiwa ni pamoja na miradi ya nyumba inayoendelea," alisema.

Sambamba na thamani ya shirika kuongezeka, Mchechu alisema mtaji wa shirika pia umeongezeka kutoka Sh. trilioni 2.9 Juni, 2019 hadi Sh. trilioni 3.4 Juni, 2022 na kwamba kutokana na mtaji huo, shirika limetumia Sh. milioni 415 kama sehemu ya kurudisha fidia kwa jamii kupitia sekta za elimu na afya. Mchechu pia alisema mapato ya shirika hilo yameendelea kuongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 257.4 kwa mwaka 2022 na kwamba mwaka 2022/23 mapato ya kodi yameongezeka hadi Sh. bilioni 90.7 kutoka bilioni 89.2 kwa mwaka 2020/21.

"Kadhalika, NHC imeendelea kupata faida kabla ya kodi na kufikia Sh. bilioni 92.9 licha ya kwamba kwa mwaka wa 2020/21 faida ilishuka kutokana na kuporomoka kwa kwa hali ya soko la nyumba nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema faida halisi iliyotokana na shughuli za shirika iliongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 60.7 mwaka 2021/22 kutoka Sh. bilioni 31.7 kwa mwaka 2020/21.

"Ongezeko hili limekwenda sambamba na ongezeko la majengo na kwa sababu hali ya soko la nyumba inaendelea kuimarika matarajio yetu ni kwamba kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 shirika litaendelea kupata faida," alisema Mchechu.

Kuhusu mwelekeo wa 2023, Mchechu alisema ili kuongeza mapato katika mwaka 2023, shirika limejipanga kendelea kukamilisha ujenzi wa miradi iliyokuwa imesimama ukiwamo mradi wa Morocco Square ambao ujenzi wake uko kwenye hatua za mwisho.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuanza kutumika rasmi mwishoni mwa Machi, mwaka huu na kwamba shirika litaendelea na utekelezaji wa mradi wa Samia Housing Scheme (SHS) katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kutekeleza mradi huo, alisema wameanza ujenzi wa nyumba 560 eneo la Kawe, Dar es Salaam.

"Pia tutaanza ujenzi wa nyumba 240 eneo la Medeli, jijini Dodoma kwa ajili ya kuuza. programu ya nyumba za Samia Housing Scheme(SHS) imelenga kutatua changamoto ya makazi bora kwa watu wa kipato cha chini na kati na tunatarajia kuwa asilimia 50 ya nyumba za program hii zitajengwa Dar es Salaam, Dodoma asilimia 20 na mikoa mingine nchini asilimia 30," alisema. Alisema programu hiyo inayotekelezwa kwa awamu itakuwa na jumla ya nyumba 5,000 zitakazogharimu takriban Sh. bilioni 466 na kwaamba programu hiyo inaenzi kazi nzuri anayoifanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuijenga nchi kiuchumi na kijamii.

Mchechu alisema NHC inatarajia kuanza ujenzi wa jengo kubwa la kisasa la kibiashara (shopping mall) jijini Dodoma ili kuwapa wakazi wa jiji hilo eneo zuri na kubwa la kujipatia huduma mbalimbali za kijamii.

Mbali na miradi hiyo, alisema shirika litaendelea na ukusanyaji madeni ya kodi ya pango la nyumba yanayofikia Sh. bilioni 21 na madeni mbalimbali yatokanayo na uuzaji wa nyumba na viwanja yanayofikia takriban Sh. bilioni 11. "Msisitizo utakuwa kuhakikisha kila anayedaiwa analipa deni lake ili kuliwezesha Shirika kuendelea kuwahudumia Watanzania wote kwa kutumia rasilimali hizi za umma," alisema.

# Uraia aliyemshtaki Makonda waibua utata

**Na Grace Gurisha**

URAIA wa mfanyabiashara Patrick Kamwelwe, aliyemfungulia kesi ya madai aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na William Malecela, umeibua utata baada ya mawakili wa wadaiwa hao kuiomba mahakama imtangaze kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa sababu wameshindwa kumpata.

Makonda na Malecela ambaye ni mmiliki blogu ya Lemutuz, walifungua maombi madogo baada ya kuwa na shaka na uraia wa Kamwelwe na kutokuwa na mali zinazohamishika nchini, kwa sababu kisheria anatakiwa kulipa gharama za uendeshaji wa shauri hilo.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na wakili wa wajibu maombi hao, Reuben Simwanza, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa.

Simwanza alidai kuwa wameshindwa kumpata Kamwelwe, hivyo wanaiomba mahakama hiyo kumtangaza kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii kwa sababu jitihada zao zimeshindikana.

"Tumefanya jitihada za kumtafuta Kamwelwe lakini imeshindikana, hivyo naiomba mahakama itupe ruhusa ili tuweze kumtangaza kwenye vyombo vya habari pamoja na kwenye mitandao ya kijamii," alidai Simwanza.

Alidai kuwa kesi ilipoitwa kwa mara ya mwisho, wakili anayemwakilisha Kamwelwe, Wabeha Kung'e, alijiondoa kwenye kesi ya msingi na kesi ndogo iliyofunguliwa.

"Kwa hivyo tunaomba tumtangaze kwenye magazeti na mitandao ya kijamii ili aweze kulipa gharama za uendeshaji wa shauri alilolifungua na tunaomba mahakama hii itumie busara ili kesi iendelee upande mmoja,"alidai Simwanza.

Desemba 8, 2022 Wakili Kung'e aliyekuwa akimwakilisha Kamwelwe alijiondoa kwa sababu mlalamikaji (mteja wake) alishindwa kumpatia maelezo sahihi ili kujibu hoja zilizotolewa na wajibu maombi (Makonda na Lemutuz).

Baada ya maelezo hayo mahakama hiyo iliahirisha shauri hilo hadi Machi Mosi, 2023 kwa ajili ya usikilizwaji mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate ambaye ndiye anayesikiliza shauri hilo.

Kamwelwe anayeishi New York, Marekani, amefungua kesi ya madai namba 234/2022 dhidi ya Makonda na Malecela maarufu kama Le Mutuz akiwataka wamlipe fidia ya Sh. milioni 247.2 kwa madai kuwa wamemdhulumu gari lake aina ya Range Rover Sport.

# Vodacom, NALA waingia ubia kuwezesha malipo kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kimataifa ya NALA iliyozaliwa Tanzania, ikijishughulisha na mfumo wa malipo duniani, imeingia makubaliano ya kushirikiana na Kampuni ya Mawasiliano ya Vodacom Tanzania kuwezesha huduma ya kutuma na kupokea fedha kimataifa (IMT).

Uamuzi huo unatarajiwa kusogeza huduma zake kwa wateja walioko nchi za Umoja wa Ulaya (EU) kutuma na kupokea fedha kwa njia rahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Kampuni ya NALA ambayo ni taasisi ya huduma za kifedha kidijitali (Fintech company), imetanua huduma zake katika Bara la Ulaya kwa kuongeza nchi 19 zilizoko barani humo baada ya kuanza kutoa huduma Marekani ikitokea Uingereza.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu na Mwanzilishi mwenza wa NALA, Benjamin Fernandes, NALA ina nia ya kuiunganisha dunia kwa kuwawezesha Waafrica wanaoishi nchi za Ulaya kutuma fedha kwenda kwenye nchi zao.

Alisema jana kuwa kwa kushirikiana na Vodacom M-Pesa, upanuzi huo unaongeza umuhimu wa kutuma na kupokea fedha kwa haraka na gharama rahisi kupitia huduma hii.

Alisema NALA inakuja kama mshirika wa muhimu sana katika wakati huu ambapo huduma za kifedha ziko kiganjani.

Alisema kampuni hizo mbili zina lengo moja la kuhakikisha utumaji pesa unakuwa wa haraka, salama, wenye kuaminika na wenye gharama nafuu nchini.

Benki ya Dunia inaeleza kwamba gharama ya kutuma pesa ni wastani wa asilimia 9 ya kile unachotuma, zaidi mifumo mingi iliyoko imekuwa na ada/gharama zilizojificha na hivyo kukosekana kwa gharama halisi ya utumaji pesa.

NALA imekuwa ikifanyia kazi juhudi za kubadilisha namna utumaji wa fedha unavyofanyika kwa kuleta huduma za wazi za kifedha.

Ofisa Mtendaji Mkuu na Mwanzilishi mwenza wa NALA, Fernandes, alisema: "Nikiwa Mtanzania, inanipa furaha kuwafikia robo ya Waafrica wenzangu wanaoishi Ulaya kwa kuwapa huduma rahisi na ya kuaminika ya kutuma fedha nyumbani.

"Kupitia Vodacom M-Pesa tunaiunganisha miundombinu na hivyo kuleta daraja la malipo kati ya nchi za Uingereza, Marekani na EU kwa ujumla tunaianganisha na Tanzania.

Mkurugenzi wa M-Commerece, Epimack Mbeteni, aliupongeza ushirikiano huo huku akiongeza kwamba unaendana na mipango ya kampuni katika kukuza huduma ya IMT.

Alisema wateja wa Vodacom M-Pesa sasa wanaweza kutuma na kupokea fedha kutoka nchi zaidi ya 200 moja kwa moja kwenda kwenye akaunti zao za M-Pesa.

# Nape ataka kampuni za simu kuwabana matapeli mtandaoni

**Na Romana Mallya**



WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, (pichani) ameiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuzichukulia hatua kampuni za mawasiliano ya simu zinazoruhusu meseji za matapeli na matangazo yanayotumwa kwa watumiaji.

Agizo hilo alilitoa juzi bungeni jijini Dodoma wakati akitoa ufafanuzi wa michango ya baadhi ya wabunge kuhusu sekta ya mawasiliano.

Alisema kwa mtoa huduma za mawasiliano ambaye ataruhusu hilo atachukuliwa hatua ikiwa ni kama suluhisho la suala hilo.

"Inatosha meseji zimekuwa nyingi na mtandao wetu kwa hali ilivyo tukiendelea kuruhusu nadhani tutakuwa hatuwatendei haki watumiaji wa huduma za mawasiliano.

"Nimepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu ongezeko la meseji za matangazo mbalimbali na za matapeli ambazo wanawatumia bila ridhaa yao," alisema.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alitaka meseji hizo zidhibitiwe huku akieleza kuwa kadri wanavyokwenda yako mambo mengi inabidi yafanyiwe kazi ikiwa ni pamoja na watoa huduma .

"Matangazo kwenye simu zetu ni mengi sana, matangazo ya kila aina yanatumwa, mkatazame kama kuna namna ya kujitoa wawe wanatutangazia kwamba mtu ambaye hataki matangazo ya namna hii piga namba hii namba yako itaondolewa," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya wabunge waliochangia taarifa hiyo wameunga mkono suala la kuzimwa kwa laini ambazo hazifanyi kazi, mchakato unaotarajia kutekelezwa mwezi huu.

# Zanzibar yajivunia ongezeko la ufaulu mitihani kidato cha nne

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imetoa tathmini ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne kwa upande wa Zanzibar huku ikibainisha kuwa ufaulu umeongezeka na idadi ya wanafunzi waliopata daraja sifuri imepungua.

Matokeo hayo ni ya wanafunzi waliofanya mtihani mwaka jana ambayo yalitangazwa hivi karibuni na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA).

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Mazizini, Zanzibar, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema licha ya kupunguza daraja sifuri watahiniwa wenye sifa za kujiunga na kidato cha tano wameongezeka ikilinganishwa na mwaka jana.

Waziri Lela alisema idadi hiyo imeongezeka kutoka wanafunzi 4,403 mwaka 2021/22 hadi kufikia wanafunzi 6,094 mwaka 2022/23 na watahiniwa wengi wamepata sifa za kujiunga na elimu ya juu.

Alisema watahiniwa 18,901 kutoka shule za Zanzibar wamefaulu kati ya wanafunzi 26,169 waliofanya mitihani hiyo ya kidato cha nne.

"Kati ya wanafunzi hao waliofaulu wasichana ni 11,414 na wavulana 7,487. Ufaulu huo umeongezeka kwa asilimia 6.1 ukilinganisha na mwaka 2021 ambao ulikuwa asilimia 66.09," alisema.

Kuhusu ubora wa ufaulu, alisema watahiniwa waliopata daraja la kwanza hadi la tatu ni 6,094 sawa na asilimia 23, daraja la nne ni 18,901 na daraja sifuri ni 7,268 sawa na asilimia 27.7.

Mkoa wa Kusini Unguja ambako anatokea Rais Dk. Samia, umejitahidi na umeondoka katika nafasi ya mwisho za mikoa mitano ya Zanzibar huku mkoa wa Kaskazini Unguja ukishika mkia katika matokeo hayo.

Pamoja na mafanikio hayo, Waziri Lela alisema bado kuna kazi ya kufanya kwa kuwa malengo ya wizara ni kuondosha daraja sifuri katika mitihani ya kidato cha nne na sita.

Katika kufikia azma hizo, alisema wizara inanunua alama A kwa masomo ya hisabati na fizikia kwa matokeo ya mitihani ya taifa ya kidato cha nne na pili kutoka kwa walimu wa masomo hayo.

Waziri Lela alisema bado kuna changamoto zinazozikabili shule za sekondari na ndiyo sababu ya kutofikiwa kwa azma hizo zikiwamo uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi, uhaba wa wasimamizi wa maabara na maktaba na ukosefu wa vyumba vya maabada na maktaba.

Changamoto nyingine, alisema ni ni utoro wa wanafunzi hali iliyoababisha wanafunzi 779 kutokufanya mitihani ya kidato cha pili na kwamba sababu kuu ni utoro na ushirikiano duni kati ya wazazi na walimu.


MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL

VACANCY ANNOUNCEMENT

Muhimbili National Hospital (MNH) is a tertiary Specialised and Super Specialist Hospital in Tanzania with bed capacity of 2,178 out of which 1,570 beds are at the Main Upanga Hospital and 608 beds are at the Mloganzila facility which is 30 km away from the main Hospital. The Hospital serves between 2,000-3,000 Outpatients and 1,500 – 2,000 Inpatients per day.

The Hospital is looking for a competent and experienced person to fill the position below for 3 years contract (renewable on mutual agreement)

**1: 0 ECONOMIST/HEALTH ECONOMIST (1 POST)**

**1:1 Duties and Responsibilities**

The Economist/Health Economist shall be stationed in the Strategy and Business Development Section and shall perform the following duties and responsibilities;-

i. Planning, budgeting and Investment
ii. Collect economic statistics and information for development of Hospital economic policy
iii. Writing of Economic/Investment and Grant Proposals
iv. Design and execute research studies on economic matters to identify and explore available economic opportunities
v. Utilize research programs on implementation of Hospital economic policies that guide effective use of economic information and resources.
vi. Evaluate and establish priorities on Hospital investment in areas of production, infrastructure and business development
vii. Pro-actively identify market access opportunities for the Hospital through effective planning and development of financially sound business proposals
viii. Effectively allocate and deploy resources including people, activities, projects and investment
ix. Consulting experts' in economics on the efficacy of policies, products and services provided by the hospital
x. Develop and present reports on economics activities of the Hospital and Communicating data in the form of presentations, technical reports, and non-technical reports.
xi. Studying the economic impact of laws and regulations and advising Management on businesses and economic decisions.
xii. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**1:2 Qualifications and Experience**

Holder of Bachelor Degree in Economics/Health Economics with Minimum of at least 3 years of working experience

Holder of a master's degree in Economics/Health Economics will be an added advantage

**1:3 Experience and Skills**

- He/she should come with at least three years of working experience in economic activities.
- Working experience in Health economics will be an added advantage
- Good understanding of the subject of economics and international relations
- Good understanding of Planning and Budgeting
- Right balance of mathematical and analytical aptitude to comprehend the economic aspects thoroughly
- Abreast with the national economic policies and its impact on the organization sector
- Fluent verbal and written communication skills
- Ability to work on multiple projects and meet deadlines
- Strong orientation to team work
- Ability to handle pressure, complex situations and problem-solving capacity
- Ability to think analytically and strategically

**1.4 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**1.5 MODE OF APPLICATION**

Assigned application letter with certified copies of academic certificates and up-to-date Curriculum Vitae (CV) with three referees with reliable contacts, postal address, e-mail, and mobile numbers should be addressed to:

**Executive Director,**
**Muhimbili National Hospital,**
**P.O.Box 65000,**
**Dar es Salaam.**

**Via the following email address:**

**Email: hrt@mnh.or.tz**

**Application Deadline: 15th February, 2023.**

217259102

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tume ya Jaji Chande ilete matokeo chanya utoaji haki

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alizindua tume ya kuangalia uboreshaji wa taasisi zinazosimamia utoaji wa haki ili kuainisha vikwazo vilivyoko pamoja na sheria ambazo zinasababisha kukwamishwa katika upatikanaji wa haki ambazo ni msingi mkubwa katika ustawi wa jamii.

Katika hafla ya uzinduzi wa tume hiyo iliyosheheni vigogo nguli katika sheria na masuala ya utawala bora ikiongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Chande Mohammed, Rais alibainisha madudu yaliyomo ndani ya taasisi hizo ambazo ni muhimu katika kuhakikisha jamii inapata haki stahiki na kwa wakati. Taasisi hizo ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Mahakama, Magereza na Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Rais aliweka bayana kwamba ndani ya taasisi hizo kuna madudu mengi ambayo yanasababisha kucheleweshwa utoaji wa haki lakini pia wanaostahili kupata haki kushindwa kuipata kwa mujibu wa sheria. Alitolea mfano wa DCEA kwamba tume hiyo imekuwa kinara katika kuwabambikia watu kesi za dawa za kulevya na matokeo yake watu kuingia katika majanga wasiyohusika nayo huku wahusika wakiendelea kula maisha.

Kadhalika katika Jeshi la Polisi, aliainisha matatizo mengi ambayo mengi yametokana na mfumo na kwamba hata akiteuliwa mkuu ambaye ni safi kiasi gani, hawezi kufanya kazi kwa ufasaha na ufanisi.


Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Rais Samia kukinyooshea kidole chombo hicho ambacho kimepewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Mara baada ya kuingia madarakani takriban miaka miwili iliyopita, Rais aliweka bayana kwamba jeshi hilo limekithiri kwa madudu yakiwamo askari kubambikia watu kesi zikiwamo za mauaji, rushwa, watu kufia mahabusu, maofisa kupoteza ushahidi wa kesi na upelelezi kuchukua muda mrefu.

Ni dhahiri kwamba Rais amedhamiria kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki kadri anavyostahili badala ya mfumo uliozoeleka wa wasiostahili kupata haki ilihali wastahilio wakiikosa. Hatua hii ilisababisha kuwapo kwa msemo kwamba mahakamani kuna sheria lakini hakuna haki, ikimaanisha kwamba mtu anaweza kupata haki hata kwa kuinunua ili mradi ana uwezo wa kifedha au kiuchumi.

Katika hili, Rais Samia anastahili pongezi kwa sababu amedhihirisha kwa vitendo kwamba haki ni hitaji la msingi kwa kila Mtanzania mradi anastahili kuipata. Kwa maneno mengine, Rais Samia amedhamiria kwa dhati kuhakikisha taasisi zote zinazohusika na utoaji haki zinafanya kazi kwa weledi huku urasimu, umangimeza na rushwa vikiwekwa kando.

Ni imani kwamba Tume ya Jaji Chande ambayo pia itashirikisha wakuu wa taasisi zilizotajwa kuwa zinahusika kukwamisha haki, itafanya kazi yake kwa weledi na hatimaye kutoa mapendekezo kama ilivyoainishwa katika hadidu rejea. Jambo la msingi, tume ipewe ushirikiano ili kukamilisha kazi yake na hatimaye Tanzania ifikie hatua ya kuwa nchi ya kupigiwa mfano katika utoaji haki duniani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tuliyoambiwa Mloganzila mazito jamani, sasa tubadili nyendo kulinda akili zetu

**KWA** kawaida mfumo wa jinsi mtu anavyoishi, ndio ambavyo una mchango mkubwa katika maisha yake ya baadaye. Pia, anaweza kusababisha ama afanikiwe au asifanikiwe .

Ni muhimu mtu anapokaa chini na kujiuliza mfumo upi wa maisha anaishi sasa. Kama anaenda kinyume, basi ni wakati muafaka abadilike na kurudi kwenye mstari, kwa mustakabali wa maisha yake ya sasa na baadaye.

Nimeligusa hilo, kutokana na tulichoelezwa umma na daktari bingwa wa magonjwa ya akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, Fileuka Ngakongwa, kuhusu ongezeko la idadi ya wagonjwa wa akili wanaopokewa, kutoka wastani wa watano hadi 25 kwa siku. Ni kwamba wagonjwa wameongezeka mara tano zaidi, au kwa tafsiri ya kisomi asilimia 500.

Kwa kurejea wataalamu, afya ni hali ya kujisikia vizuri kimwili, kiakili, kiroho na kiutu bila kusumbuliwa na ugonjwa wowote, ni vyema hayo yakazingatiwa.

Vilevile wataalamu wa afya wanasema, dawa za kulevya ni kemikali inayoingia mwilini na kuathiri ubongo wa mtumiaji, hata kumsababishia nyendo batili kutokea matendo, hisia, fikra kutoka kwenye mwongozo wa akili.

Dk. Ngakongwa anataja visababishi vya ugonjwa wa akili ni ulevi wa pombe, kutumia dawa za kulevya kama bangi na heroin, sehemu kubwa ya wanaopokewa hospitalini hapo, wanabainika kitabibu walitumia vilevi hivyo. Pia, anataja kichocheo kingine ni msongo wa mawazo, tatizo la hisia na wasiwasi uliopitiliza, kwamba vyote hivyo vinaweza kusababisha ugonjwa wa akili.

Kwa kuwa matumizi ya dawa za kulevya yametajwa kuwa miongoni mwa visababishi vya ugonjwa wa akili, nadhani kuna haja sasa kwa jamii kubadili mfumo wa maisha na kushiriki katika vita dhidi ya matumizi ya dawa hizo.

Jamii inaweza kushiriki katika vita hivyo, kwa kutoa taarifa biashara ya dawa za kulevya inakofanyika na wahusika wakuu, iwe rahisi kuwanasa wahusika, wanaowaharibu watu kusababisha wajiingize katika matumizi ya dawa hizo.

Njia hiyo ya kushirikiana na serikali katika vita ya dawa za kulevya inaweza kusaidia watu kubadili mfumo wa maisha yao, kutoka kwenye mazingira hatarishi hadi yaliyo salama.

Ni maoni yangu, taarifa hizo za Mloganzila zisaidie kubadilisha mfumo wa maisha ya jamii, kwa kila mmoja wetu kutambua madhara ya dawa hizo na hata pombe, ili waepuke matumizi yake, hatimaye kulinda afya zao.

Ushirikiano huo unafaa kujumuisha, utoaji elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya na pombe, ubadilishaji tabia za wale ambao walikuwa na mpango wa kujiingiza huko na hata wanaotumia waweze kubadilika.

Siku ya Kimataifa ya Afya ya Akili, huadhimishwa kila Oktoba 10 ya mwaka na kaulimbiu stahiki ni kutokomeza vyanzo vya tatizo hilo. Siku hiyo isaidie kuleta matokeo chanya hasa kwa jamii kutambua umuhimu wa kulinda afya.

Mfano hai, ni kwenye maadhimisho ya mwaka jana, yalinogeshwa na kaulimbiu "Fanya afya ya akili na ustawi kwa wote kipaumbele cha kimataifa."

Ina maana kwamba, hiyo ni hali ya kuwa sawa kiakili na kisaikolojia au kutokuwapo usumbufu wa akili ya mtu kwamba inakuwa msongo wa mawazo.

Hivyo, jambo la ushiriki wa kila mmoja katika vita dhidi ya dawa za kulevya na utoaji elimu stahiki ya afya, vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika vita hiyo.

Takwimu za kimataifa kupitia ujumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Akili Duniani mwaka jana, ni kwamba wastani wa watu bilioni moja duniani kote wanaishi na matatizo ya akili.

Hapo anaelekeza hatua stahiki zichukuliwe, kuhakikisha kunakuwapo huduma bora ya afya ya akili kwa wote, ili kuboresha afya ya akili, pia kuwapo mkakati wa kuunusuru umma kutoka katika janga hilo.

Inaelezwa kuwa, afya ya binadamu itakuwa njema kama jamii itafuatilia kanuni na taratibu bora za afya, pasipo kusahau suala la mlo kamili.

HABARI KITAIFA

# Kamati Bunge yabaini udumavu wa samaki

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imesema utafiti unaonyesha katika Bwawa la Mtera lililoko Mpwapwa mkoani Dodoma, samaki wamepungua lakini waliopo wamekumbwa na udumavu.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma (pichani) aliyasema hayo juzi bungeni wakati akiwasilisha taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na kamati hiyo katika kipindi cha Februari 2022 hadi Januari, mwaka huu.



Dk. Ishengoma alisema utafiti unaonyesha kupungua kwa kiwango kikubwa cha samaki katika maziwa, mabwawa na mito nchini kutokana na usimamizi hafifu wa raslimali hizo.

Alisema katika Ziwa Victoria, samaki wazazi ni chini ya asilimia nne na katika Bwawa la Mtera samaki wamepungua lakini waliopo wamekumbwa na udumavu.

"Kwa kuwa, hali hiyo imeathiri upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya kusindika minofu ya samaki, watu kupoteza ajira, kukosekana kwa lishe na kuvuruga uchumi wa wavuvi, Bunge linaishauri serikali kuwekeza kwenye utafiti na teknolojia ya uzalishaji wa samaki na viumbe maji wengine. Serikali iwezeshe TAFIRI (Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania) kupata meli ya uvuvi ili kutekeleza majukumu ya kiutafiti katika Ukanda wa Maji ya Bahari," alisema.

Pia alisema itenge fedha na kuhamasisha na kuwawezesha wafugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika mabwawa na maziwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki pamoja na kudhibiti uvuvi haramu kwa kutumia njia sahihi ambazo hazitwezi utu wa wananchi lakini zinaleta matokeo chanya.

"Ihamasishe sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa samaki na vyakula vya samaki," alisema.

Pia alishauri serikali iimarishe huduma za ugani kwa kuwapatia maofisa ugani utaalamu na vifaa vya ukuzaji wa viumbe maji kwani wananchi wamehamasika kufuga samaki kwenye vizimba lakini hakuna wataalamu wa kutosha kuwasaidia mbinu bora za ufugaji.

"Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Kitengo cha Kulinda uhifadhi wa raslimali za Uvuvi baharini "Marine park reserve unit" ili kukiwezesha kitengo hicho kusimamia uhifadhi wa raslimali za uvuvi katika maji baridi kwa lengo la kulinda sehemu za mazalia ya samaki,' alisema.

Alisema mapendekezo hayo yanatokana na ukweli kwamba, kitengo hicho kilifanikiwa kwa sehemu kubwa kudhibiti uvuvi wa kutumia mabomu katika Bahari ya Hindi.

Akichangia taarifa hiyo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Kunti Majala alisema alihoji kama Kamati imesema kuna udumavu wa samaki kuna athari gani kwa wanaokula kitoweo hicho.

"Je, sisi tunaokula wanakuaje? Tujiandae na sisi kuwa wadumavu wa afya kwa sababu tunachokula kinajaza tumbo hatuli chakula bora tuna lishe duni, ndiyo maana tunaona hapa, sijui ni kwa sababu ya udumavu wa samaki ndio maana tunaambiwa," alisema.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akitoa ufafanuzi wa hoja hiyo wakati muda wa mbunge huyo ukiwa umekwisha baada ya kupewa dakika moja na Spika, alisema mbunge Kunti ameiongezea chumvi hoja hiyo.

"Anasema kama samaki wanadumaa, na sisi tutadumaa pia, kesi iliyoibuliwa na Mheshimiwa Kiswaga (Jackson) imeeleza kwamba katika bwawa la Mtera ipo mito inayoingiza maji kwenye bwawa lile.

"Kuna wakulima wanaonekana wanatumia kemikali, zinapoingia kwenye maji zinasababisha kudumaa au kutokuwa sawasawa kwa samaki, si kwamba ni samaki wote," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema: "Si samaki wote, hoja ninadhani ni ya kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti si ipo kwenye taarfa zenu (ndio), ipo kwenye taarifa ya kamati, Mheshimiwa Ulega hii ipo kwenye taarifa ya kamati na wao wameeleza mahususi, nadhani wamesema Mtera, hata wao hawajasema samaki wote, wabunge wanazungumzia samaki waliodumaa Mtera."

Baada ya maelezo, Ulega alisema amekubaliana na hoja ya kamati ambayo inazungumzia Bwawa la Mtera na kuahidi kwenda kufanya utafiti na kuja na hatua za kuondoa tatizo hilo.

Mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka jana, Nipashe iliandika habari ikiangazia shida zianzoikabili jamii ya Mtera wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma kutokana na kuadimika kwa samaki kwenye bwawa hilo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mtera, Angela Minja alisema licha ya mabadiliko ya nchi kuathiri upatikanaji wa samaki kwenye bwawa hilo, shida nyingine ni matumizi ya nyavu zinazoitwa 'timba' ambazo hutumika kwenye uvuvi haramu na kusababisha uhaba huo.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **STICK UP AUCTION MART, J&J RECOVERIES, JADA INVESTMENT LIMITED na HOLLYNESS AND RESPISHERS CO. LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | STICK UP AUCTION MART | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | LUCIANA L FRANCES | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIYEGEYA-MOROGORO |
| 2 | STEPHANO E SABUNI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | FOREST- MOROGORO |
| 3 | AMINA S SALUMU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYANDIRA-MOROGORO |
| 4 | AFROGIANT INSURANCE AGENCY LTD | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIRANYI-ARUSHA |
| J&J RECOVERIES | | | |
| 5 | GRANT R MUSHI | VIWANJA VIWILI VYENYE MKATABA WA MAUZIANO KIMOJA MALI YA MDHAMINI- BAKARI ISSA KONGELA | MZINGA NA MASEYU-MOROGORO |
| 6 | ALLY SHABANI KITONGE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | UBENA- ZOMOZI-CHALINZE |
| 7 | HUSSEN SALUM KIPARAMOTO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKUNDI-KIHONDA-MOROGORO |
| JADA INVESTMENT LIMITED | | | |
| 8 | GLORY REMMY SWAY | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KUNGURU-GOBA-DAR ES SALAAM |
| 9 | HONEST K HUBERT | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | CHAMA-DARAJANI-DAR ES SALAAM |
| 10 | JOEL GEORGE NDAOMBWA | KIWANJA CHENYE MSINGI CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MADALE-KISAUKE-DAR ES SALAAM |
| 11 | SUBIRA JAMES JOHN | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KINYAMWEZI-DAR ES SALAAM |
| 12 | FATMA M MWILU | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | GALAGAZA NA ZOGOALI-DAR ES SALAAM |
| 13 | AMANI P DAUDI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NZASA-ZINGIWA-DAR ES SALAAM |
| 14 | TANDI SAMU SIKALANGWE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI MALI YA ALLY HAMISI KAHEMERA | MZINGA-KITUNDA-DAR ES SALAAM |
| 15 | EVAR B MTWEVE | VUWANJA VIWILI VYENYE MKATABA WA MAUZIANO | VIANZI NA MLALENI-DAR ES SALAAM |
| | HOLLYNESS AND RESPISHERS CO.LTD | | |
| 16 | EBELINO B MWALONGO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | LYOTO-MBEYA |
| 17 | MWILE Y MWASHIBANDA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBALIZI - MBEYA |
| 18 | BURTON CHOMBE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA: 219 KITALU D | MBALIZI - MBEYA |
| 19 | JANKEN MWALENGO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | TONYA- MBEYA |
| 20 | ELIAS MWAKASEKELE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IWINDI –VETA- MBEYA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Stick Up Mart**
**S.L.P Arusha**
**Namba za simu: 0786559593**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**J&J Recoveries**
**S.L.P Dar Es Salaam**
**Namba za simu: 0714292260**

**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Jada Investment Limited**
**S.L.P Dar es Salaam**
**Namba za simu; 0788493699**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Hollynes and Respishers Co.Ltd**
**S.L.P Mbeya**
**Namba za simu: 0762058614**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**

217258901

# Kamati tathmini uchumi wa vyombo vya habari yanena

**Na Christina Mwakangale**

KAMATI ya Kutathmini Hali ya Uchumi wa Vyombo vya Habari nchini imezinduliwa rasmi huku mwenyekiti wake, Tido Mhando, akiahidi kutoa mapendekezo yatakayotekelezeka kwa ustawi wa tasnia hiyo.

Tido alitoa ahadi hiyo juzi mkoani Dar es Salaam baada ya kamati hiyo kuzinduliwa rasmi huku akisema matarajio ya kamati hiyo ni kufanyiwa kazi kwa mapendekezo itakayotoa na kuondoa wasiwasi miongoni mwa wanatasnia na Watanzania kwa ujumla.

"Ninakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri (Nape Nnauye) alipoteua kamati hii, baadhi ya waandishi wa habari waliuliza 'mbona walioteuliwa wote viongozi? Hatudhani kama wanaelewa hali halisi ya yale ambayo waandishi wa habari wanapitia'.

"Ninaomba niwahahakishie waandishi wenzetu kwamba sote tumepitia huko, sisi kwanza tunaumia sana. Ni sawa sawa na mwenye nyumba au baba, ndiye mlezi inafika sikukuu huwezi kununua chakula, ada ya shule huwezi kulipa, inakuumiza sana.

"Hakuna wakati unakuwa mgumu unapofika mwisho wa mwezi, una wafanyakazi, unatakiwa kuwakarimu na huna uwezo huo. Sisi tumeweka dhamira kwamba yote tutakayoyapendeza yanatimizika," alisema Tido ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa Azam Media.

Alikiri kuwa hali ni mbaya kiuchumi kwa vyombo vya habari vingi nchini, akisisitiza kuna haja hatua zichukuliwe kunusuru hali hiyo.

Tido alisema kuundwa kwa kamati hiyo ni faraja kubwa kwa sekta ya habari nchini, akibainisha kwamba vipo baadhi ya vyombo vya habari vimeshindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi kwa kipindi kirefu.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, akimkaribisha mgeni rasmi wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo, alisema kuwa baada ya kuundwa kwa kamati hiyo, matumaini ya waandishi wa habari ni makubwa kutokana na kikwazo cha uchumi kilichoko kwenye tasnia hiyo.

"Changamoto zimefikia kutishia uhai wa vyombo vya habari. Kwa hiyo, kamati hii imejenga matumaini kwa waandishi wa habari na wawekezaji wa sekta hii ya habari," alisema Msigwa ambaye pia ni Katibu wa Kamati hiyo.

Awali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Khamis Abdulla, alisema kamati hiyo inatarajiwa kufanya kazi kwa ufanisi na kuja na suluhisho dhidi ya matatizo kwenye sekta hiyo.

Alisema wanatarajia kamati hiyo itapata taarifa za waandishi wa habari walioajiriwa na wasio na mikataba na wawakilishi mikoani kwa kufahamu vipato vyao na kupatikana suluhisho katika sekta hiyo.

Kamati hiyo iliyoundwa Januari 24, mwaka huu, na Waziri Nape. Mbali na Tido na Msigwa, wajumbe wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile, Mkuu wa Maudhui Clouds Media Group, Sebastiana Mganga.

Wengine ni Mtendaji Mkuu wa Mwananchi Communications, Bakari Machumu; Mkurugenzi Mtendaji wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Keneth Simbaya; Mkurugenzi Mtendaji wa Multichoice Tanzania, Jackline Woiso na Mwandishi wa Habari mzoefu, Richard Mwaikenda.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Hashim Komba (kulia), akikabidhi nyaraka za kazi kwa Mkuu mpya wa Wilaya hiyo, Mohamed Moyo, wakati wa hafla ya makabidhiano ya ofisi wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa Katoliki laiburuza CCM kortini

**Na Kulwa Mzee**

KANISA Katoliki Jimbo la Kigoma limefungua shauri Mahakama Kuu kupinga Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kigoma kuchukua eneo la kanisa bila ridhaa yake.

Shauri hilo limefunguliwa chini ya hati ya dharura katika Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma na limepangwa kutajwa mbele ya Jaji Lameck Mlacha.

Walioshtakiwa katika shauri hilo ni Bodi ya Wadhamini ya CCM, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waombaji katika shauri hilo wanadai mjibu maombi namba mbili, Wizara na Halmashauri ya Uvinza, wamepanga kuchukua eneo lao kuipa CCM bila ridhaa yake kwa ajili ya kujenga madarasa ya Shule ya Sekondari ya Chumvi.

Kanisa Katoliki wanaiomba Mahakama ikubali kutoa amri ya zuio la muda kwa wajibu maombi na mawakala wao au watu wengine kujenga au kuendeleza eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 39.6.

Inadaiwa eneo hilo linalobishaniwa liko jirani na eneo lingine la mwombaji lenye ekari 21.4 lenye hati namba 4231 na liko Kijiji cha Nyambutwe, Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Mwombaji anaomba Mahakama iamuru wajibu maombi wasifanye kitu chochote katika eneo hilo hadi shauri la msingi litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Kanisa Katoliki katika maombi hayo, limewasilisha hati tatu za viapo zilizoapwa na Padri Experius Hamenyande, Christopher Mibanda na Emmanuel Kimpanti.

Katika viapo vyao, Padri Hamenyande anadai mwaka 1920 Kanisa Katoliki waliomba eneo kwa kiongozi wa jadi wakati huo wakapewa ekari 61 maeneo ya Nyambutwe kwa ajili ya kujenga kanisa, shule, nyumba za watumishi, kituo cha afya na kuacha eneo lingine kwa ajili ya makaburi.

Wanadai mwaka 1934 ekari 21.4 zilipimwa na kupewa hati namba 4231, eneo ambalo halikupimwa ekari 39.6 liliendelea kubakia chini ya kanisa.

Mwaka 2020, CCM waliomba eneo hilo kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Chumvi lakini walikataliwa.

Inadaiwa Januari 4, 2021 Kanisa Katoliki liliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM wakitaka shule hiyo ihamishwe kutoka kwenye ardhi ya mgogoro lakini hilo halikufanyika.

Inadaiwa Julai mwaka 2022 Waziri wa Ardhi kupitia barua yenye kumbukumbu namba CBA 166/171/01/57 alitoa maelekezo kwa Kanisa na Katibu Mkuu wa CCM akihimiza chama hicho kuhamisha miundombinu yao kwenye eneo lenye hati miliki ya kanisa.

"Alielekeza Halmashauri ya Uvinza iandae mpango wa matumizi ya ardhi kwenye eneo ambalo halijapimwa na ligawiwe kwa watu wengine. Waziri alielekeza eneo la makaburi lisitumike kwa maziko, maelekezo hayo yalichochea mgogoro," alidai Padri Hamenyande katika kiapo chake.

Waombaji wanadai hawakukubaliana na uamuzi huo wanaona hawakutendewa haki, wanaomba Mahakama ikubali maombi yao. Mahakama imepanga shauri hilo litajwe Februari 15, mwaka huu.

# DC Moyo aomba ushirikiano

**Na Steven William,** NACHINGWEA

MKUU mpya wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, amewaomba viongozi na wananchi kumpa ushirikiano katika utendaji kazi ili kuiletea maendeleo.

Moyo aliyasema hayo juzi alipofika kuripoti wakati akitokea Wilaya ya Iringa ambako alikuwa akifanya kazi mwanzoni alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu.

Alisema kuwa anaomba ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wenzake, watumishi, madiwani, viongozi wa chama, wananchi na wazee ili kuhakikisha anafanikisha wilaya kukua kiuchumi na kukuza maendeleo kwa wananchi.

Mkuu huyo wa wilaya aliwahakikishia wananchi wa wilaya hiyo kuwa nao bega kwa bega na milango iko wazi wakati wowote kusikiliza kero zao.

Alisema kuwa ametokea CCM na yuko tayari kuhakikisha anatekeleza vilivyo ilani ya Chama Cha Mapinduzi ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea aliyehamishwa, Hashim Komba, alikabidhi ofisi kwa Moyo huku akisema anakabidhi wilaya kwa mikono miwili ikiwa salama kabisa na watu wa Nachingwea ni wachapakazi na wakarimu.

Komba alisema anawashukuru watumishi wa idara zote, wananchi na wazee na viongozi wa CCM, Kamati ya Ulinzi na usalama kwa kumpa ushirikiano kwa muda wote aliokaa Nachingwea.



# W'biashara Soko la Samunge wapewa msaada mil.100/-

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KIONGOZI wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, Dk. GeorDavie Kasambale amekabidhi stakabadhi ya malipo ya benki ya Sh. milioni 100, aliyoahidi kwa wafanyabiashara wa Soko la Samunge, Jijini Arusha.

Fedha hizo ni kwa ajili ya kuwafuta machozi wafanyabiashara waliopoteza mali na mitaji yao mwaka 2019, kutokana na ajali ya moto iliyoteketeza soko hilo na kuwaacha masikini.

Katika fedha hizo, Sh. milioni 20 zitatumika kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya soko hilo na kuweka milango na ujenzi wa miundombinu ya mifereji ya majitaka.

Kabla ya makabidhiano hayo kwa Mwenyekiti wa Soko la Samunge, Sekela Ntondolo, Dk. GeoDavie, aliwapa somo wafanyabiashara hao kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili kujikwamua kiuchumi.

Kwenye nasaha zake, Nabii huyo aliwasihi wafanyabiashara hao kufanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Fanyeni yale yanayowapasa kwa nguvu zote na msimuingize shetani kwenye pesa hii, ambayo nimeitoa. Mungu amenipa mimi uwezo na ndio maana na mimi nawasaidia wahitaji kama ninyi wafabiashara,"alisema.

Baada ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa wafanyabiashara, Njola Miraji, alimshukuru kiongozi huyo wa dini kwa kutimiza ahadi yake.

"Fedha hii tutaigawa kwa wafanyabiashara 1,261 wa soko hili. Kati ya wafanyabiashara hao wako wafanyabiashara wa vyombo 95, mama lishe 86, vyakula vikavu 56, viongozi 23, wafanyabiashara wa viatu 85 ,wafanyabiashara wa nguo 397 na wa mboga 519,"alisema.

Mwenyekiti wa soko hilo, Restuta Nyoni, aliwasihi wafanyabiashara hao ambao watapata fedha hizo kuziingiza katika mitaji yao huku akiwasisitiza kutotumia fedha hizo kufanya anasa.

# AKO kutekeleza miradi ya mil.490/- sekta ya elimu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MIRADI mipya ya ujenzi wa shule na uboreshaji wa miundombinu ya sekta ya elimu katika Wilaya za Hai na Moshi, mkoani Kilimanjaro, inayotekelezwa na Shirika la AKO Tanzania Community Support, italigharimu Sh. milioni 490.

Dk.GeorDavie alitoa ahadi hiyo Januari 23 mwaka huu katika soko hilo, baada ya kupokea ombi kutoka kwa wafanyabiashara hao juu ya uhitaji wa mitaji iliyopotea kutokana na kuunguliwa kwa soko hilo mwaka 2019 na kupoteza mali zao . Jana, Mkurugenzi wa shirika hilo, Hilda Kimathi, alisema katika Wilaya ya Hai, miradi mipya ya ujenzi ni shule jumuishi ya wenye ulemavu inayojengwa katika Shule ya Msingi Kibaoni, kwa gharama ya Sh. milioni 100.

Zingine ni Shule ya Msingi Darajani, unatekelezwa mradi wa ujenzi vyumba viwili vya madarasa, choo cha wanafunzi na walimu pamoja na ofisi ya walimu, ambavyo vyote vitaigharimu Sh.milioni 150.

Mwingine ni mradi wa ujenzi wa jiko la kisasa, vyumba vya madarasa na ofisi za walimu katika Shule ya Msingi Uchau iliyoko Moshi Vijijini ambao utaigharimu Sh. milioni 240.

"Miongoni mwa sababu ambazo zimetusukuma kutekeleza miradi hii ya elimu ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na kukosekana kwa miundombinu rafiki katika shule zetu. Jambo ambalo tunaona limekuwa likichangia kushuka kwa kiwango cha elimu nchini.

"Shule nyingi za serikali zinatishiwa na uchakavu wa miundombinu yake, ndiyo maana tumeamua kuweka mkono wetu kuunga mkono serikali na kuwatua mzigo wa kuchangia gharama za ukarabati wananchi wa maeneo hayo yatakayonufaika."

Miradi mingine ambayo inatekelezwa na AKO Tanzania Community Support katika eneo la Moshi Vijijini ni ukarabati wa shule tatu chakavu za msingi, zilizokuwa zikihatarisha maisha ya wanafunzi na walimu kutokana na vyumba vya madarasa kukatika nyufa na kuharibika vibaya miundombinu yake.

Miradi hiyo pia inaigharimu AKO Tanzania Community Support, Sh. milioni 350, inazihusisha Shule ya Msingi Sungu, Shule ya Msingi Kibosho na Shule ya Msingi Singachini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, AKO Tanzania Community Support, inatekeleza mradi wa ukarabati wa Shule ya Msingi Sungu (Sh. milioni 100), Shule ya Msingi Kibosho (Sh. milioni 50) na Shule ya Msingi Singachini (Sh. milioni 200).

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uchau, Agness Mbwambo alisema: "Tumepata mradi kutoka Shirika la AKO Tanzania Community Support, wametujengea jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na walimu. Kabla ya mradi huu, chakula kilikuwa kikipikwa katika vyumba vya madarasa." Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Hans Simmer, alisema AKO Tanzania Community Support, imejikita kusaidiana na jamii, kukarabati shule za msingi ambazo hali ya majengo yake ni mbaya ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.



Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Jacob Kimeso (katikati), akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la kupitia taarifa za kata zao 18, wilayani humo juzi. Kulia ni Ofisa Utumishi wa Halmashauri hiyo, Dominica Ngaleka na Katibu wa UWT wa Wilaya hiyo, Leokadia Fissoo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Japan yajitosa kufadhili mtambo wa kuchuja floride

**Na Allan Isack,** ARUMERU

JAPAN imejitosa kufadhili mtambo maalum wa kuchuja maji yenye madini ya floride kabla ya matumizi, ili kuwasaidia wananchi wa Lemanda katika Kata ya Oldonyosambu, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha waliokuwa wakipata tabu kwa miaka mingi.

Tafiti za kisayansi zinaonyesha kuwa 'floride' ni madini yenye madhara makubwa kwenye mifupa, uti wa mgongo na meno kuwa kahawia na kuyafanya yasiwe magumu.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuzindua na kukabidhi mradi huo, Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yashushi Misawa, alisema Japan imefikia hatua hiyo baada ya kugunduliwa kiasi kikubwa cha madini hayo kwenye maji, ambayo yanatumiwa na wananchi hao.

"Utafiti unaonyesha kwamba maji ya eneo hilo yana madini ya floride yaliyozidi miligramu 24 kwa lita moja, ambayo yana madhara kwa binadamu.

"Lakini mtambo uliofungwa katika eneo la mradi, utaondoa madini hayo mpaka kufika miligramu 0.1 kwa lita. Kiasi ambacho kinakubalika kimataifa kwa matumizi ya binadamu," alieleza Balozi Misawa.

Alisema uwapo wa mtambo huo utasaidia kuondoa tatizo la watoto wanaozaliwa kupinda miguu, mgongo kuwa na vichwa vikubwa na kuharibika meno.


Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru, James Mchembe, akizungumza katika hafla hiyo alisema Tanzania inatambua na kuthamini juhudi na mchango unaotolewa na za Serikali ya Japan kwa Watanzania.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ili kudumisha ushirikiano huo kwa lengo la kutatua matatizo ya kijamii nchini.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung'u Salekwa, alisema mtambo huo utakuwa neema ya kipekee wananchi wa Lemanda na aliomba ubalozi huo kuangalia namna ya kuongeza mtambo ambao utawafikia wananchi wa vitongoji vyote vitatu vyenye tatizo kama hilo.

Akisoma risala ya wananchi wa Lemanda, Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Lomunyaki Ndiyogi, alisema kuwapo kwa tatizo hilo kumewaathiri watoto kwa kushindwa kutembea kwenda shuleni.

Mtambo huo wa kuchuja maji umetengenezwa na Chuo Kikuu cha Shunshi cha Japan, una uwezo wa kuzalisha lita 300 kwa saa na kuhudumia wananchi zaidi ya 400 wa Kitongoji cha Lemanda umegharimu Dola za Marekani 115,000 (Sh. milioni 264).





# Waogopa kueleza tatizo la ugonjwa kisa mavazi ya kijeshi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WANANCHI wa Kata ya Nyahanga Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wanaogopa kueleza ugonjwa unaowasumbua mbele ya wataalamu wa afya katika Zahanati ya Jeshi la Polisi kutokana na wahudumu kuvaa sare za jeshi.

Zahanati hiyo inatoa huduma ya mama na mtoto, maabara, uzazi wa mpango na kliniki kwa ajili ya watoto wadogo chini ya miaka mitano.

Zahanati hiyo imesaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Kahama hususani wagonjwa wa nje (OPD) wanaotoka mikoa mbalimbali ikiwemo Geita, Tabora, Kigoma na maeneo ya Wilaya ya Shinyanga.

Diwani wa Nyahanga, Helena Bundala aliyabainisha hayo jana katika mkutano wa hadhara wa kusoma mapato na matumizi ya kata hiyo uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Nyahanga A.

Alisema wajawazito wengi wanafika katika zahanati hiyo kupata huduma kulinganisha na wale wanaofika Hospitali ya Wilaya.

Alisema wagonjwa wengi wanaofika katika zahanati hiyo kupata matibabu, wamekuwa wakiingiwa na hofu baada ya kuhudumiwa na muuguzi aliyevaa sare za Jeshi la Polisi hali ambayo baadhi yao wamekuwa wakishindwa kujieleza anachoumwa na wakati mwingine wamekuwa wagumu kusubiria majibu baada ya kutoka maabara.

"Sisi kinamama tunatembea tukiwa na madeni ya vikoba sasa tunapofika zahanati ya polisi kutibiwa kwa kuepuka msongamano wa wagonjwa Hospitali ya Wilaya tunawaogopa wauguzi wakiwa wamevalia sare za polisi, hivyo wawe wanavaa mavazi ya kidaktari ili tuwaeleze vyema kile kinachotusumbua," alisema Bundala.

Kadhalika, alisema hata kama sheria inawataka kuvaa sare za polisi wakati wakitoa huduma kwa wagonjwa ni vyema wakavaa nguo za kidaktari mara mbili kwa wiki hususani siku za kliniki kwa wajawazito na watoto wadogo ili kuwaondolea hofu.

Fatuma Mohamed mkazi wa eneo hilo, alisema kipindi chote cha ujauzito wake alikuwa anahudhuria kliniki katika zahanati hiyo kujua maendeleo ya mtoto wake.

Alisema baada ya kujifungua pia aliendelea kuhudhuria kliniki ya mtoto wake na wanapata matibabu vyema kama ilivyo katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Diwani wa kata hiyo, Pancras Ikongoli aliwaomba wananchi kuondoa hofu wanapofika kupata matibabu ya kiafya na hivi karibuni wanatarajia kupandisha zahanati hiyo kuwa kituo cha afya cha kata na kitakuwa kinaendeshwa na halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Akijibu hoja hili Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Dk. James Luhaja, alikiri wauguzi wake kutoa huduma kwa wagonjwa wakiwa wamevalia mavazi ya Jeshi la Polisi na kusema kuwa atahakikisha analisimamia hilo japo wawe wanavaa sare za kidaktari mara tatu kwa wiki kwani hakuna sheria inayowataka kutoa huduma wakiwa wamevalia nguo hizo za kijeshi.

Alisema wagonjwa wanazidi kuongezeka kila siku hali ambayo imewafanya kuomba kuongezewa watumishi watano kati ya hao, madaktari wawili, mtalaamu wa maabara mmoja na wahudumu wawili na maombi hayo wameyafikisha ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

Akisoma mapato na matumizi, Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Nyahanga, Ellen Mugenyi alisema wamekusanya na kutumia Sh. milioni 1.13 ambazo walizielekeza katika ukarabati wa choo cha walimu katika Shule ya Msingi Nyahanga A.

Alisema shule hiyo haikuwa na choo na walimu walilazimika kwenda kujisaidia katika choo cha walimu shule jirani ya Nyahanga"B".



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kanda ya Ziwa, George Mhina (kushoto), akiwa na wanafunzi wa shule ya sekondari Kabela Gold, wakifungua maji, wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji shuleni hapo, wilayani Kahama juzi, unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) na kufadhiliwa na EWURA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani matatani madai ya kumwozesha mwanafunzi

**Na Vitus Audax,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kumsaka na kumtia mbaroni Diwani wa Kata ya Ibwera iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani humo kwa tuhuma za kushirikiana na wazazi kumuozesha mwanafunzi wa darasa la sita.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi kwa kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo wakati akiwaapisha wakuu wa wilaya walioteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan na kusema kuwa diwani huyo amekuwa akishiriki kuwatetea wazazi hao pindi wanapoulizwa juu ya upotevu wa mwanafunzi huyo.

Aidha, alisema mwanafunzi huyo ambaye jina lake limehifadhiwa alikuwa akisoma katika Shule ya Msingi ya Bubaga na kwamba alitoroshwa kwa ajili ya kuozeshwa katika Wilaya ya Karagwe.

Alisema wazazi wa mtoto huyo wakiulizwa wanasema yupo mkoani Mwanza ilihali yupo wilayani karagwe baada ya kuachishwa masomo yake na kupokea mahari sambamba na kufungishwa ndoa huku diwani huyo akidaiwa kujua kila kitu.

"Katika suala hili diwani anajua lakini 'anafurukuta' kuwatetea wazazi hawa polisi kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya mtafuteni Diwani wa Ibwera mkamateni na hatua za kisheria zitumike," alisema.

Katika hatua nyingine Chalamila alilitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua wazazi wanaofanya udanganyifu kwa kuchukua RB wakidai kupotelewa na watoto kwa ajili ya kupoteza ushahidi baada ya kuozesha.

"Huo mchezo wa RB kwa sasa umekuwa wa uhongo wakidai kuwa wanapeleka taarifa kituo cha polisi ili kujivua tuhuma hizo kumbe wamemtorosha, wamemuozesha, ni mjamzito na hawachukui majukumu yoyote," alisema.

# EWURA yakoshwa na matumizi ya fedha KUWASSA

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Ziwa imeridhishwa na utekelezaji wa fedha zilizotumiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama (KUWASSA) kwa ajili ya kurejesha huduma kwa jamii (CSR).

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina alipokagua utekelezaji wa miradi katika Shule ya Sekondari ya Kabela Gold iliyopo katika Kata ya Mwine na Shule ya Sekondari Bugisha iliyopo katika Kata ya Mwenda Kulima wilayani Kahama.

Mhina alieleza kuwa Marchi mwaka 2022, EWURA ilitoa Sh.milioni 15 kwa KUWASSA kama tuzo baada ya kuibuka mshindi wa pili kati ya mamlaka 26 za mkoa zilizopitiwa na kushindanishwa katika utoaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mbali ya Shule ya Sekondari ya Kabela Gold, nyingine zilizonufaika na fedha hizo ni Shule za Sekondari Bugisha, Mama Kalembo na shule ya watoto yenye uhitaji maalum ya Mwine na zaidi ya wanafunzi 1,500 walinufaika na mpango huo.

Wakieleza kwa nyakati tofauti walimu wakuu wa shule za Bugisha na Kaleba walishukuru EWURA kwa kupeleka huduma ya maji katika shule hizo kwa kuwa imesaidia kupunguza utoro wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya shule kwa kupanda miti na usafi wa vyoo na madarasa.

Kwa upande wa wanafunzi wameeleza kuwa upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama shuleni umewasaidia kuepukana na magonjwa.

Akizungumzia msaada huo, Mhandisi Maginge Marwa kutoka KUWASSA alisema shule zilizonufaika na mradi huo ni zile zilizopo umbali wa zaidi ya kilomita moja kutoka bomba kuu la KUWASSA linapopita.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 2, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mazingira; ajenda ya Rais Samia akiishikilia kila kona tangu kuapa**



Ukurasa 13

**MJUE FRANK CHAMBIKA**
Balozi Fistula CCBRT anayevuma kazini, akiguswa na yaliyomkuta mzazi wake



Ukurasa 14

**TOCHI YA WASOMI:**
**Ulivyo uzuri wa maua majumbani na angalizo lao 'hatari ya sumu'**

UUZAJI KUNI, MKAA, MILUNDA NA MAGOGO...

# Kukosekana mbadala wenye nguvu kwaweka rehani mazingira Kisarawe




Sehemu ya mandhari ya wilaya ya Kisarawe, iliyotawaliwa na misitu. **PICHA: MAKTABA**

**Na Amri Lugungulo,** Kisarawe

INAPOTAJWA Kisarawe, inarejewa wilaya ya kimazingira inayotawaliwa na utajiri wa misitu, pia mimea. Hapo nako kibinadamu shughuli za kuchoma mkaa, pia ukataji mkubwa wa kuni, magogo na miti ya kujengea choo, maarufu milunda zimetawala.

Zao lake, ni tishio la eneo hilo kutokea jangwa, kutokana na uharibifu wa mazingira unaotokana na kukata miti ovyo.

Jamii mbalimbali huvuna mazao ya misitu wilayani hapa wakiegemea madai ya kujikwamua kiuchumi, pasipo kupewa uzito athari za uharibifu, zikiwamo zinazosababisha ukame.

Inatajwa hadi sasa kuna shehena nyingi za mazao hayo husafirishwa kwenda mkoani Dar es Salaam, ambako wako wanunuzi wengi, ikizingatiwa ni wilaya iliyo jirani na mkoa mkuu wa kibiashara kitaifa.

Kinachofanyika kutoka Kisarawe, ni kwamba wavunaji hukusanya mazao yao na kisha wachuuzi wanayafuata huko huko misituni. Hapo zinatajwa bidhaa kama kuni, mbao, mkaa na magogo, wanayasomba kwa magari na pikipiki na wakati mwingine huyasogeza kando ya barabara yakibebwa na mabasi ya abiria.

Uzoefu unaonyesha ni hali inayozua hoja kinzani, baadhi ya abiria wa mabasi wakisikika kulalamika wanachafuliwa na vumbi la mkaa yanayobebwa kwenye mabasi. Kwa kifupi, si hali rafiki kwa usafiri wa umma.

Mkaa huo unaopakiwa kwenye magunia, maarufu viroba, huingizwa na kufichwa ama chini ya viti vya abiria au kwenye sehemu ya kuweka mizigo ya abiria na hupita kwenye vituo vya ukaguzi, pasipo kukaguliwa na mamlaka husika.

Sasa kuna kikundi kilichojitokeza kukagua walakini huo unajitokeza kwenye huduma tajwa. Abdallah Mijayo na Seifu Mkali na wezao wengine wameanzisha Shirika la Maendeleo la Utunzaji wa Mazingira Tanzania (CMT) Wilaya Kisarawe.

Mijayo, ambaye ni mwenyekiti wa shirika hilo, anasema uharibifu wa misitu wilayani humo, umeshamiri kiasi cha kuwalazimisha wao kujitokeza kujinusuru na hali hiyo, kwa njia mbadala ya nishati.

Anasema, mtazamo ni haja ya watu wabadilike ili kuepukana na uharibifu unaotishia jangwa wilayani humo.

Mijayo anasema, hofu ya uharibifu huo imezidi kupanda kutokana na ushuhuda wa shehena za magunia ya mkaa, kuni, magogo na milunda kusombwa kuelekea Dar es salaam.

Anasema kwamba, hilo linawalazimisha kuanzisha shirika hilo, ili kuwahamasisha watu kuacha matumizi ya mkaa na kuni, badala yake wabadilike na kuanza kutumia nishati safi ya gesi.

**OFISA MISITU ANENA**

Kaimu Ofisa Misitu wilayani Kisarawe, Waziri Mkumbwa, anasema mwaka jana zaidi ya magunia 121,000 sawa na tani 60,000 za mkaa, pia kuni mita za ujazo 51,000; pamoja na ujazo wa mita 770 za magogo; na mita 10,000 za milunda, vyote vilibebwa kwenda jijini Dar es slaam.

Aidha, inatajwa kwamba kuna wastani wa pikipiki 150 zinazobeba magunia matatu makubwa kila moja kutoka wilayani hapa kila siku, kwenda Dar es Saaam.

Mkumbwa anaeleza kwamba, ni mazao yanayoongoza kwa kulipatia kipato kwa asiimia 68 wilaya hiyo, licha ya kwamba yanaharibu mazingira husika.

**SEMINA YA KUWANOA**

Hivi karibuni, shirika hilo la utunzaji mazingira liliitisha semina ya siku moja mjini Kisarawe, kujadili utunzaji wa mazingira kwa wakati mkaa na watengenezaji wa majiko ya mkaa.

Ni kazi ya kitaaluma iliyoandaliwa na shirika hilo likishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Shule Kuu ya Uchumi, ambako washiriki wakaiomba serikali kupunguza bei ya gesi, ili kuongeza idadi ya watumiaji wake, hali inayowapunguza watumiaji kuni na mkaa.

Pia, wakaiomba serikali kutoa elimu ya matumizi ya gesi kwenye shule na kwenye makazi ya watu, ili kuepukana na ajali zinazoweza kusababishwa na matumizi ya nishati hiyo. Maombi hayo wameyatoa, baada ya mwezeshaji wa semina kuutaka umma ubadilike kwa kutumia nishati safi na salama.

Mtaalamu mwezeshaji, Dk. Onesmo Selejio, anatoa angalizo kwamba matumizi ya kuni na mkaa ni hatari kwa afya ya mtumiaji, kwani moshi wa mkaa una sumu na zinazidi kuwapo kila matumizi ya mkaa na kuni, zinavyoongezeka.

Kitaifa inaelezwa, hadi sasa asilimia 64 ni watumiaji mkaa; asilimia 26 wanatumia kuni; asilimia tano wako kwenye gesi; asilimia tatu umeme; wakati asilimia mbili zilizobaki ziko katika nishati nyinginezo.

Dk. Selejio anatahadharisha kuwa, afya ya wananchi itakuwa salama, endapo umma utabadilika kwa kutumia nishati safi, ikiwamo ya gesi.

" Mkaa na kuni zina sumu hivyo hakuna usalama kwa watumiaji," anasisitiza.

MAZINGIRA

# Mazingira; ajenda ya Rais Samia akiishikilia kila kona tangu kuapa



Rais Samia Suluhu Hassan, alipokutana na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Joyce Msuya, mwaka juzi Ikulu Dodoma. Katikati Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwaandishi Wetu**

TANGU mwaka 1995 nchini, sekta ya mazingira nchini imekuwa ikipewa uzito ikiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ni mwendelezo wa mtazamo na mikakati mbalimbali ya kimazingira, tangu kupatikana uhuru wa nchi.

Kwa mujibu wa tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, inaanika kupatikana muungano uliounda Tanzania, kutoka Tanganyika na Unguja, mazingira ikijumuisha mambo muhimu ya kuyashughulikia kimuungano.

"Mazingira ni sehemu ya mikakati minne ya maendeleo ya kujenga manufaa sawa yanayohusu manufaa ya kiuchumi na kijamii, pasipo kuathiri maslahi ya kizazi kijacho,"inafafanua sehemu ya maelezo hayo.

Hadi sasa inatajwa kusimamia masuala ya mazingira na hapo ndiyo imechangia mwaka 1997 kuanzishwa sera yake, pia mwaka 2004 kukapitishwa Sheria ya Taifa ya Kusimamia Mazingira. Zao lake, inatajwa kuibuliwa mipango na miradi mbalimbali ya mazingira, ufahamu mpana na elimu inayohusiana nayo.

Daima, dhana utekelezaji na usimamizi wake umekuwa ukiendelezwa kitaifa katika awamu tofauti za kiutawala nchini, ikiwamo ya sasa.

**ZAMA ZA SAMIA**

Rais Samia Suluhu Hassan, anafafanua umuhimu wa kuwa na namna shirikishi ya kutafutia majibu ya mahitaji yanayojitokeza, akihimza haja ya ushirikiano madhubuti kijamii, katika utunzaji mazingira nchini na ugenini.

Kwenye Mkutano wa 20 wa Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati (AMECEA), uliofanyika Dar es Salaam, Julai mwaka jana, Rais Samia akasisitiza wajibu wa kila mtu kutunza mazingira, hivyo ni vyema kuwapo ushiriki wa pamoja.

> "Niwaombe sana kuendelea kushirikiana na serikali, kama mnavyofanya sasa katika kuendeleza mapambano ya uharibifu wa mazingira...

Anarejea mtazamo mpana wa hoja akitaja maandiko ya kidini, nayo yanasisitiza utunzaji mazingira, hivyo akawaomba viongozi hao kushirikiana na serikali kuandaa mikakati ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

"Niwaombe sana kuendelea kushirikiana na serikali, kama mnavyofanya sasa katika kuendeleza mapambano ya uharibifu wa mazingira..." anasema Rais Samia

Anadokeza madhara ya mazingira, akitahadharisha kuwa magonjwa mengi ya mlipuko ni zao la uchafu, unaosababishwa na mazingira kutotunzwa kwa usahihi.

Pia, anaitaka sekta binafsi kuiga mfano wa viongozi wa dini kuwa mstari wa mbele kwenye utunzaji mazingira, akitoa wito kwa viongozi mbalimbali katika maeneo yao kuhakikisha wanasimamia na utunzaji wa mazingira, pasipo kuchoka.

Ni fursa hiyo, Rais akaupongeza mkoa wa Dar es Salaam kushika nafasi ya sita kwa usafi barani Afrika, huku naye akipokea pongezi za na wito kutunza mazingira kutoka kwa Papa Francisko.

Rais Samia, anawataka viongozi wa kidini na kisiasa, kuthamini na kuyajali mazingira, akinena:"Dunia ndiyo nyumba yetu sote pamoja. Hakika sisi hapa Tanzania tunathamini maisha ya kijamii yanayoendana na mkakati huo wa Kanisa Katoliki, kwamba sasa tuijenge nyumba yetu sote."

**KWANINI MAZINGIRA?**

Katika mjumuiko wake na viongozi hao wa dini, Rais Samia anawaambia kuwapo amani katika jamii, kunasaidia kukabili ikolojia na uharibifu wa mazingira, kama vile ukataji miti unaoathiri hali ya hewa duniani.

Hapo anadokeza athari za kina cha bahari, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuyalinda mazingira, ili kutohatarisha maendeleo kwa ujumla, muhimu ni kutunza vyanzo vya maji na misitu, kupanda miti na kulinda maeneo yanayoizunguka jamii, kama yanavyoelekezwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira.

Rais Samia ambaye kabla ya wadihfa wa sasa, alikuwa Makamu wa Rais, nafasi yenye mamlaka na kusimamia mazingira, anasema hadi sasa serikali inafuata siasa ya maendeleo jumuishi, hivyo ipo tayari kuzipokea na kufanya kazi na taasisi zisizo za kiserikali, zikiwamo za kidini.

Hadi sasa nchini kuna sera, pia sheria Shirikishi ya Umma na Binafsi. Rais Samia anaendelea:"Niwaombe serikali yenu ni sikivu, ni serikali inayopokea! Leteni maoni yenu kwenye utunzaji mazingira, tukae kwenye vikao."

**ALIKOANZA MKAKATI**

Kipindi kifupi tangu aingie madarakani, Rais Samia katika tukio la kuwaapisha wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa, moja ya maagizo ya wajibu aliyowapa ni kuhakikisha wanatunza mazingira katika maeneo ya uongozi wao.

Katika tukio Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma, Rais akawatamkia viongozi hao na wa taasisi mbalimbali, akiwaagiza "kasimamieni mazingira yetu ya Tanzania kwa sababu mazingira yetu ndio uhai wetu."

Vilevile, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, mwenye dhamana na ustawi wa mazingira katika tukio hilo, akasisitiza:"Wajibu wa viongozi hawa ni kuhakikisha mazingira yanakuwa endelevu."

Miezi michache baadaye, Rais Samia akakutana na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Joyce Msuya jijini hapo, akimuahidi kushirikiana katika mipango ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini. Rais akaiomba UNEP katika Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Miaka Mitano waliokuwa wanaanada wakati huo mnamo Julai 2021, uwe endelevu na wenye kuleta tija katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini.

**MAJALIWA ASIMAMIA**

Ni katika mwaka huo 2021, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, mwezi mmoja kabla ya Rais Samia kukutana na bosi wa UNEP, akaziagiza taasisi nchini kuanza kuingia kwenye nishati mbadala kuachana na kuni.

Akiwa ni mtendaji mkuu wa kiserikali nchini, Majaliwa, akaziagiza wizara, taasisi na mashirika yote ya kiserikali na sekta binafsi, pia vikundi vya uzalishaji zinazotumia nishati ya kuni na mkaa, zianze kutumia nishati mbadala kwa kupikia na shughuli nyingine za uzalishaji.

Ni tamko alilotoa Juni Mosi, 2021, kwenye maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani, zilizofanyika kwenye ukumbi wa Hazina, jijini Dodoma, akitoa mfano wa taasisi kama shule, vyuo, hospitali na majengo makubwa zinapaswa kuzingatia ufungaji mifumo ya nishati ya gesi kwa ajili ya kupikia.

"Kila wizara ifanye ufuatiliaji kwenye taasisi zake na nipatiwe taarifa ya hali ya utekelezaji kila baada ya miezi sita, inayoonyesha ni taasisi ngapi zimefikiwa, zimebadili mifumo au zimejenga majengo kwa kuzingatia hitaji la nishati mbadala.

Waziri Mkuu akawataka viongozi wa jiji la Dodoma, wahakikishe wanaweka mkakati ya maeneo yote yanayopimwa, yapandwe miti na kila anayepata kiwanja aelimishwe umuhimu wa kupanda miti.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, katika hilo akaahidi kuifanyika semina kwa maofisa mazingira kutoka Ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) walemishwe dhana hiyo.

"Maofisa mazingira hawa hawakuwa wanatumika vizuri, kupitia maadhimisho haya tutabadilishana mawazo na kujua nini cha kwenda kufanya kuhusu ajenda ya mazingira," anasema, akidokzea itaendana na kampeni mahsusi ya itakayohusisha wadau mbalimbali wa maendeleo katika mtazamo endelevu.

AFYA

MJUE FRANK CHAMBIKA

# Balozi Fistula CCBRT anayevuma kazini, akiguswa na yaliyomkuta mzazi wake

**Na Mwandishi Wetu**

UGONJWA fistula ya uzazi nchini, kama ilivyo kwingineko, umeshika sana maisha ya jamii. Ni kuwapo tundu lisilo la kawaida kati ya njia ya uzazi na kibofu cha mkojo au njia ya haja kubwa ya mwanamke, ikisababishwa na uchungu wa muda mrefu na uzazi pingamizi, pasipo msaada wa haraka.

Katika sekta ya afya nchini, vita inapiganwa vilivyo kuikabili na moja ya wadau wakubwa, ni Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam, pia kuna vita vya mtu mmoja mmoja.

Mzazi mwenye fistula hutokwa na haja ndogo au kubwa, au vyote kwa pamoja kupitia faragha yake, akikosa uwezo kujizuia. Ni hali inayomdhalilisha, hata anashindwa kushiriki shughuli za kijamii, wakati mwingine anatengwa na mume au familia.

Nchini, inakadiriwa wanawake 2400 wanaishi na fistula na wengine kati ya 1500 hadi 3000 hupata fistula ya uzazi kila mwaka. Kati yao, wanaotibiwa kwa mwaka ni chini ya 1400. Hivyo, maelfu ya wanawake wenye fistula hubakia katika jamii wakiteseka.

Matibabu yake nayo yamekuwa magumu nchini, kutokana na sababu nyingi, zikiwamo kukosekana taarifa sahihi za matibabu hayo yasiyo na malipo.

Hapo kuna simulizi ya hela za matibabu, unyanyapaa na imani potofu, kuwa fistula ya uzazi inasababishwa na kulogwa, laana na mwanamke kufanya mapenzi na wanaume wengi wakati wa ujauzito.

CCBRT ilianza kutibu fistula mwaka 2003 na ilipofika 2012, ikaanzisha mradi rasmi kuhamasisha na kutibu, kukiwapo mabalozi maalum wa kuhamasisha tiba.

Kimsingi, Balozi wa Fistula wa CCBRT, ni mtu atokaye kwenye jamii au mhudumu afya, aliyepatiwa mafunzo ya namna ya kuwabaini wagonjwa hao, akawafikisha katika kituo maalumu cha matibabu, kama ilivyo Hospitali ya CCBRT au washirika wengine.

Mnamo Juni ya mwaka 2013, mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Mama Salma Kikwete, alizindua kampeni za kuhamasisha matibabu ya fistula akitoa wito: Hakuna mwanamke hata mmoja anayetakiwa kuishi na hali hiyo ya udhalilishaji inayomuondolea hadhi na utu wake."

Mradi wa Fistula wa CCBRT, unalenga kuboresha afya na elimu ya wanawake wanaoishi na fistula ya uzazi nchini, kwa kuwahamasisha watibiwe na kuondoa vikwazo vikuu vitatu vinavyowazuia matibabu yao: Gharama za usafiri kwenda hospitali; ukosefu elimu yake; ugumu wa kupata matibabu, na dhana potofu kuhusu fistula.

Tangu mwaka 2003, CCBRT na hospitali washirika imetoa matibabu kwa kinamama zaidi ya 10,000 waliokuwa na fistula. Inatajwa, idadi hiyo ni ndogo, ikilinganishwa na ukubwa wa tatizo kitaifa.

Nipashe imezungumza na balozi katika vita vya kukabili shida fistula, Frank Chambika (35), mwenye maelezo lukuki. Fuatilia mazungumzo yao ya ana kwa ana:

***SWALI:*** Tueleze historia ya maisha yako?

***JIBU:*** Nilizaliwa mwaka 1988 katika kijiji cha Miangalua wilaya ya Sumbawanga vijijini, mkoa wa Rukwa. Mimi ni mjasiriamali na mkulima mdogo mwenye elimu ya kidato cha nne. Nina mke na watoto wanne, ambao hivi sasa wanaendelea na masomo ya elimu ya msingi kijijini kwetu.

***SWALI:*** Ulikutana wapi na CCBRT?

***JIBU:*** Hapo awali nilikuwa nafanya kazi za kujitolea kwenye shirika moja la lishe, ambako tulikuwa tunafanya kazi za kuelimisha jamii juu ya masuala ya lishe bora. Baada ya mradi huo kumalizika, wakapendekeza jina langu kwa CCBRT na huo ulikuwa mwaka 2015. Nikapatiwa mafunzo na CCBRT, wakatufundisha namna ambavyo tunaweza kuwabaini wagonjwa wa fistula katika jamii, kisha kuwasafirisha kwenda CCBRT Dar es Salaam kwa matibabu.

> **Tangu mwaka 2003, CCBRT na hospitali washirika imetoa matibabu kwa kinamama zaidi ya 10,000 waliokuwa na fistula. Inatajwa, idadi hiyo ni ndogo, ikilinganishwa na ukubwa wa tatizo kitaifa.**

***SWALI:*** Tangu wakati huo hadi sasa, umeleta wagonjwa wangapi wa fistula kwa matibabu?

***JIBU:*** Kumbukumbu zangu zinaonyesha zaidi ya kinamama 400 kutoka mkoani Rukwa wamepitia katika mikono yangu kwa kipindi cha miaka saba iliyopita na mwaka jana, yaani 2022 nimeleta wagonjwa 28 nikiwa balozi wa fistula, aliyeleta wagonjwa wengi mwaka uliopita.

***SWALI:*** Kinamama 28? Hongera sana! Nimeelezwa wewe ndiye kinara wa kuleta wagonjwa wengi kwa mwaka jana hiyo ni idadi kubwa au ndogo kwako?

***JIBU:*** Kwangu mimi naona hiyo ni idadi ndogo, maana mwaka jana sikuweza kufanya kazi vizuri, kwani nilikuwa namuuguza mtoto wangu kwa takribani kipindi cha miezi sita.

***SWALI:*** Wewe ni mjasiriamali na kazi hii ya kutafuta wagonjwa unajitolea, kitu gani kinakupa msukumo na unagawaje muda wako wa kutafuta riziki na wakati huohuo kupita kwenye jamii kutafuta wagonjwa?

***JIBU:*** Kusema kweli, kazi ya kutafuta hawa wagonjwa ni ya kujitolea, nami niliguswa sana baada ya mama yangu mzazi kupata ugonjwa huu, wakati huo hatukujua chanzo chake ilikuwa ni nini na wala hatukuwa na taarifa kuwa ugonjwa huu unatibika. Yalikuwa ni mambo ya kienyeji tu.

Nilipokuja kuambiwa habari za fistula, nikaihusisha moja kwa moja na ugonjwa wa marehemu mama yangu na huo ndio ukawa msukumo wa kujitolea kuwasaidia kinamama wanaoteseka na 'gonjwa' hili.

Kuhusu suala la muda, mimi hutenga muda wa wiki mbili kwa mwezi na kuanza kuzungunga katika vijiji nyumba kwa nyumba na katika magulio, zahanati na mikusanyiko mingine, nikifanya uhamasishaji pale ninapo pata taarifa ya mgonjwa na kudhibitisha kuwa ndiye hufanya mawasiliano na CCBRT, wananitumia nauli nafanya mpango wa kumsafirisha.

***SWALI:*** Changmoto gani unakumbana nazo katika kazi yako hii ya kutafuta wagonjwa?

***JIBU:*** Ziko nyingi, ila nitaje chache;kwanza ni usafiri, ujue huko kwetu vijijini barabara ni mbaya sana za vumbi, matope wakati wa mvua, madaraja mabovu na vijiji vingine viko mbalimbali sana.

Bila ya usafiri walau wa pikipiki, huwezi kufika sehemu waliko wagonjwa. Kumbuka, wengi wao wanapatikana vijiji vya ndani, ambako wakati mwingine huduma za afya ziko mbali.

Pili ni suala la utambulisho. Kuna wakati tunakuwa na changamoto ya kutambulika, kama kweli sisi tunafanya kazi na CCBRT, kwa maana hatuna vitambulisho rasmi, mbali na vipeperushi vyenye nembo ya CCBRT na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Binafsi nilipata barua kutoka kwa Mkurugenzi na DMO (Ofisa Afya wa Wilaya ), ambayo inanitambulisha mimi ni nani nnapokuwa kwenye jamii, kuwashawishi wagonjwa hadi wakubali kupanda gari kuja Dar es Salaam kutibiwa, ni kazi kubwa sana.

Unakuta mtu tangu anazaliwa hajawahi kutoka nje ya wilaya yake, leo hii unamueleza suala la kusafiri kuja Dar es Salaam, binafsi hiyo hunipa wakati mgumu sana.

***SWALI:*** Nini ombi lako?

***JIBU:*** Ombi langu kwa wahusika wa mradi, yaani CCBRT wajitahidi hasa watupatie usafiri walau pikipiki moja kila wilaya, ili kama mabalozi tuwe tunapeana zamu kuichukua pale kwa DMO na kwenda kutafuta wagonjwa vijijini, kwani naweza kusema usafiri ndiyo changamoto kubwa ya upatikanaji wagonjwa.

Pia, tuwe na utambulisho rasmi. Suala la posho ya motisha au 'incentive' kama ambavyo wao huita tunashukuru kuanzia mwezi Novemba mwaka 2022 walipandisha posho hiyo kutoka 10,000 hadi 20,000 pale balozi anafanikiwa kumpata na kumsafirisha mgonjwa.



Mkurugenzi wa Rasilimaliwatu wa Hospitali ya CCBRT (kushoto), Anastasia Melis na Meneja Miradi, Yohana Kasawala (kulia), wakimpongeza Balozi wa Fistula kutoka Sumbawanga Vijijini, Frank Chambika, aliyeshika cheti cha umahiri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**INAENDELEA UK.14**

MAZINGIRA

TOCHI YA WASOMI:

# Ulivyo uzuri wa maua majumbani na angalizo lao 'hatari ya sumu'

**Na Mwandishi Wetu**

MAUA na nyasi daima zinapendeza kupandwa majumbani ni sehemu ya nyenzo za kupendeza majumbani. Inapotajwa mimea hiyo, iko ya aina mbalimbali kwenye makazi, ziko za staili kuanzia upenuni hadi mabarazani.

Washauri wa kitaalamu wana maoni, kwamba maua na mimea hutunzwa katika muda wa ziada, ikiwa na manufaa kwa kuwajengea wakazi wastarehe na wahisi furaha na kupunguza msongo wa mawazo.

Kila mtu akitaka kupanda maua, huchagua kwa kuangalia uzuri wa mwonekano na harufu, pasipo kujali madhara ya kiafya ya maua husika. Mtazamo mpana unafikia penye watoto wadogo wengi; mimea inatajwa kuwa nyongeza nzuri binafsi, iwe ndani au nje.



Maua yaliyopendezeshwa kwenye mandhari ya nyumba. **PICHA: MTANDAO**

## FAIDA ZA MAUA

Zao la kwanza, mtu anapata hewa safi na ya asili. Pia, anapata sehemu nzuri ya kupumzikia nje ya nyumba yake, ikiendana na kupendezesha mwonekano wa ndani na nje ya nyumba.

Ni hali inayosaidia kupangilia na kuainisha matumizi mazuri ya ardhi ya nje, pia maua hupunguza msongo wa mawazo kwa uzuri wake, ikileta burudani ya macho kwa mtazamaji.

Kuna baadhi ya maua yanatajwa nayo ni hatari kuwa nayo. Inatajwa, iwapo mtu awe mzazi mama au baba, hata mzoefu katika ulimwengu wa maua, miti na mitishamba basi angalizo hilo linamhusu.

Ingawa yanaweza kuonekana yenye kuvutia kwa harufu, bado yaweza kuleta mauti. Baadhi ni sumu kwa wanyama, mfano, paka wanaweza kuteseka kutokana na kudhurika figo au hata kuchangia kifo.

Hivyo, ni busara mtu kuboresha mandhari ya kijani kibichi isiyo na madhara kwa jamii wakazi na wanyama waliopo au yanayoweza kujitokeza.

Kuna aina mbalimbali za maua yenye sumu, ambayo yanaweza kudhuru, au hata kuua kwa wanadamu na wanyama wanaioshi nao, pale yakimezwa au kuguswa.

Kwa kuzingatia yote hayo, ni muhimu mtu akajielimisha madhara ambayo maua yenye sumu yanaweza kuwa nayo kwa afya zetu na wanyama pia.

> **Zaidi, maua mengine huleta matatizo ya kuwashwa na magonjwa mengi ya ngozi kwa watu watakaoyagusa, hapo ikiwajumuisha hata watu wazima.**

## YAKOJE MADHARA?

Haipendekezwi kuwekwa maua ndani ya nyumba na ikiwa kuna watoto majumbani wanaoyala kwa bahati mbaya, huwa ni hatari kwa afya zao.

Baadhi ya maua yanatajwa si rafiki kwa afya za binadamu, hasa watoto wadogo. Kisaikolojia, watoto wanatajwa wanapenda kuyashika na kuchezea maua, hata kuyalamba na kuyaweka mdomoni. Hiyo kiafya, inaelezwa kwamba inaweza kuleta madhara kwao.

Zaidi, maua mengine huleta matatizo ya kuwashwa na magonjwa mengi ya ngozi kwa watu watakaoyagusa, hapo ikiwajumuisha hata watu wazima.

Baadhi ya maua yanayojulikana na kwa sumu kali ni pamoja na 'matumbawe' ya msimu wa baridi, pia huitwa: Cherry ya Matumbawe; Lavender ya usiku; Oleander, ambayo pia inajulikana kama 'Plum ya Willow', na manukato ya kifaransa jasmine.

Maua ya Ole kwa Kifaransa au Plum ya Willow, huwa na matawi na majani yanayopendeza. Mara nyingi, yanaonekana katika bustani au mikanda ya kijani.

Kuna watu wanaopenda kukaa nyumbani kufanya kazi ya mapambo, kwenye maeneo yao, barazani hadi kwenye sufuria.

Hapo ndipo kuna Oleander, mmea wenye sumu kali, unaosababisha hata vifo kwa wanadamu na wanyama, ikiwa italiwa kimakosa; ni mmea, uliojaa sumu, hasa penye shina lake na majani.

Sifa ya kuweka maua nyumbani, daima haishii katika hali ya kuchanua vizuri, ni zaidi ya hapo ama madhara au usalama kiafya .

## NINI KIFANYIKE?

Inatajwa kwamba ni lazima kwenye kila nyumba, kabla ya kupandwa maua kwenye jengo, jambo muhimu la kuanza ni kufanyika utafiti kupata usalama wake, ndipo upandaji unapochukua nafasi.

Sura ya utafiti inapanuka, hata kupata maoni kuhusi ufafanuzi wa usalama wa maua hayo kutoka kwa majirani wanaokuzunguka.

## FAIDA ZA KUTAFITI

Hapo inatajwa baadhi ya faida za kufanyika utafiti na kupata taarifa kamili juu ya usalama wa maua unayotaka kupanda nyumbani kwako.

Faida moja, ni ama kupunguza au kuepuka baadhi ya magonjwa, hasa kwa matatizo ya ngozi maarufu kwa jina la mzio (allergy). Pia, inasaidia kuepuka madhara ya afya za watoto, wasichezee na kushika kwa mikono, halafu kulamba au kwenda kula bila ya kunawa mikono vizuri.

Manufaa hayo hufikia hatua ya kunusuru afya ya wanyama wanaoishi hapo, huku inaisaidia jamii kuwa na uhakika wa usalama wa vitu. Kitaalamu, inatangazwa jamii kuwa na uchaguzi sahihi wa aina ya maua wanayoyapanda majumbani na muhimu katika hilo kuwalinda wanyama wao wanaowafuga.

Hivyo, ni lazima wapandaji maua hayo kufanya utafiti mdogo ili kujua aina ipi ya maua inaweza kufaa kupandwa katika maeneo yao ya kuishi hasa kuzunguka nyumba.

Hiyo inatajwa itasaidia kupunguza madhara ya kiafya yatokanayo na maua. Baadhi ya athari hizo ni kuwashwa na baada kuyagusa au kuwadhuru watoto, baada ya kuyagusa na kuweka mdomoni.

***• Waandishi ni; Dk. Mourice Victor (0784864417) Mhadhiri katika Taasisi ya Dawa Asili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili na Pankras Luoga (0757645746), Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya, ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***

# Balozi Fistula - CCBRT anayeng'ara, akiguswa na yaliyomkuta mzazi wake

**INATOKA UK.13**

## DARASA LA MABALOZI

Ijumaa wiki iliyopita, Hospitali ya CCBRT iliyoko Msasani, Dar es Salaam, iliendesha mafunzo kwa mabalozi wa fistula zaidi ya 100 nchini kote, Bara na Visiwani. Frank Chambika, kutoka mkoani Rukwa, ni miongoni mwa wahudhuriaji, aliyeng'ara kwa kuleta wagonjwa wengi zaidi.

Ni mafunzo yaliyolenga kuwakutanisha wabadilishane uzoefu, changamoto na namna ya kukabiliana nazo. Pia, inagusa kuwakumbusha mbinu za kutambua na hatimaye kuwafikisha wagonjwa katika vituo vya kutoa huduma.

Baada ya kugundua kinamama wengi wenye tatizo hilo na jamii inayowazunguka, hawana uelewa mzuri juu ya ugonjwa huu na upatikanaji wa matibabu yake,.

hospitali hiyo inatumia mtandao wa mabalozi kutafuta wagonjwa wa fistula katika jamii.

Mbinu nyingine inajumuisha radio za mikoa na kitaifa, vipeperushi, mikutano ya uhamasishaji jamii na mafunzo mbalimbali, ujumbe mfupi wa simu za mkononi, pia matangazo ya televisheni na magazeti.



# Ufaransa yafungua ubalozi mdogo mkoani Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UBALOZI wa Ufaransa umefungua ofisi ndogo mkoani Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mbalimbali.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa ofisi hiyo juzi jijini hapo, alisema tukio hilo ni sehemu ya jitihada zinazofanywa na Rais Samia katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

Dk. Tax alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada katika kuimarisha ushirikiano na mataifa mbalimbali pamoja na masuala ya kidiplomasia.

"Leo hii tumekuwa na tukio la ufunguzi wa ofisi ya kuanzia ya ubalozi wa Ufaransa hapa Dodoma tunawashukuru sana kwa tukio hili lakini haya ni matokeo ya Rais Samia na jitihada zake za kutaka kuimarisha ushirikiano na mataifa mbalimbali na kurahisisha mawasiliano kati ya serikali yetu na mataifa mengine,"alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu mbalimbali mkoani hapa ili kuwezesha mabalozi ambao watakuwa tayari kuhamia kupata huduma zote bila kikwazo.

"Nilipoambiwa manakuja leo na mnatumia uwanja huu wa ndege nikasema msifikilie kuwa huu ndiyo uwanja pekee tulio nao hapana tunajenga uwanja mkubwa sana wa ndege Msalato lakini pia tunaendelea kuboresha huduma nyingine kama vile ujenzi wa barabara,reli ,shule pamoja na huduma nyingine za kijamii ambazo mtaweza kuzitumia mkihamia hapa,"alisema.

Kadhalika, aliwataka mabalozi kuunga mkono jitihada za serikali kuhamia makao makuu Dodoma kwa kuanzisha ofisi zao na serikali itakuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kufanikisha jambo hilo.

"Niwahakikishie kuwa serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itaendelea kutoa ushirikiano mtakao uhitaji muda wote lakini pia kwa balozi ambazo zitakuwa tayari kutaka kufungua ofisi zao jijini Dodoma tutazisaidia kufanya hivyo"alisema

Hata hivyo Dk. Tax alisema serikali inatambua jitihada mbalimbali za kimaendeleo ambazo zimekuwa zikifanywa na ubalozi huo nchini katika sekta za nishati,maji pamoja na usafirishaji.

Naye, Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania Nabil Hajloui, alisema ufunguzi wa ofisi hiyo ni matunda ya Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea ofisi ya ubalozi huo alipofanya ziara mwaka jana nchini Ufaransa.

Alisema mataifa ya Tanzania na Ufaransa yamekuwa na ushirikiano wa kidiplomasia kwa muda mrefu hivyo kufunguliwa kwa ofisi hiyo ndogo jijini Dodoma kutaendeleza kuimarisha mahusinano yaliyopo kimataifa.

# 'Taasisi za umma hazina mkataba huduma kwa mteja'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKUU wa shule za sekondari zinazomilikiwa na taasisi za dini nchini wametakiwa kusimamia maadili ya wanafunzi na walimu ili kuwa na kizazi chenye maadili.

Msaidizi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Deogratius Msanya aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa wakuu hao ulioandaliwa na Kamisheni ya Huduma za Jamii ya Kikristo (CSSC).

Alisema jambo kubwa linalosumbua kwa sasa ni maadili kwa wanafunzi na walimu, hivyo kuna haja ya wakuu hao kupaza sauti ili kukomesha vitendo hivyo. "Mtoto ambaye amejengwa kwenye misingi ya kiimani na kimaadili atakuwa vizuri na atakuwa na hofu ya Mungu na hata mahali pa kazi utaona utendaji kazi wake utakuwa ni wa hali ya kujali na ataonesha kuwajali wale anaowahudumia," alisema.

Alisema kama kuna mambo yasiyo mazuri ni vyema kuchukua hatua za haraka kushughulika ili kutokuwa na kizazi chenye shida baadaye.

Hata hivyo aliishauri serikali kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali ambazo zinajitokeza katika jamii ikiwamo suala la ukosefu wa maadili na vitendo ambavyo havimpendezi Mungu.

"Changamoto naona ni utandawazi taarifa zipo kiganjani wanafunzi wanajifunza mambo mengi sana, watoto kuwapa simu wakiwa na umri mdogo nayo ni shida, ukweli tungependa sana shule zetu zisitajwe kwenye mambo kama hayo wakuu wa shule zetu angalieni elimu yenye maadili," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CSSC, Peter Maduki, alisema taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 1992 kwa ajili ya kuimarisha huduma za utoaji wa elimu na afya zinazotolewa na taasisi za kanisa.

Alisema wana taasisi za elimu 1,033 ambazo zimesajiliwa na serikali katika ngazi ya elimu ya awali msingi, sekondari vyuo vya kati, ufundi na vyuo vikuu. Alibainisha ili elimu iwe bora wanashughulikia suala la maadili kwa kufuata sera ya ulinzi wa mtoto na kufundisha elimu ya dini kwa wanafunzi na mafunzo ya kanuni za kazi na maadili kwa walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanalelewa katika misingi ambayo wanatarajiwa na jamii.

Alisema wanajaribu kuimarisha mafunzo ya dini ili wanafunzi waishi kulingana na maadili na wanakuwa na upendo kuwaepusha kwenda kinyume na msingi wa kanisa.

"Tumenzisha klabu za ulinzi wa watoto shuleni ili waweze kuelimishana juu ya mambo hayo, wito wangu kwa jamii na wazazi, malezi lazima yahusishe jamii nzima malezi mazuri yanatolewa nyumbani wasiwaachie walimu peke yao," alisema Maduki. Mkuu wa Idara ya Elimu Baraza la Maskofu Tanzania (TEC), Sista Joyce Mboya, alisema kupitia mkutano huo wamejifunza kuhusu malezi kwa vijana na watahakikisha shule wanazozisimamia kwa vitendo. "Ndio maana sisi tuna sera inayotuongoza na tuna vitabu vya kufundishia ili wakienda popote waweze kufanya kazi wawe wawajibikaji na wabunifu kwa ajili ya kuendeleza taifa," alisema.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akiwa na mgeni wake, Waziri wa Finland anayeshughulikia masuala ya uchumi, Mika Lintila, baada ya kumaliza mazungumzo ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chamwino yapokea mapendekezo ongezeko bajeti

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dk. Semistatus Mashimba amepokea mapendekezo ya baraza la madiwani kuhusu kuongezwa kwa bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha wa 2023/24 ya Sh.bilioni 3.5.

Dk. Mashimba alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema kuwa halmashauri imekubali kuhusu mapendekezo hayo ya madiwani ya kutaka kuongeza fedha katika bajeti hiyo ya mapato na matumizi kwa kuwa itaenda kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi kwenye sekta mbalimbali.

Alisema nyongeza hiyo itawezesha kuwahudumia wananchi kwa asilimia 100, kimaendeleo kupitia miradi inayotekelezwa na ile ambayo itakayoanzishwa kwenye maeneo yao.

"Halmashauri yetu kwa asilimia 100, hatuna sababu ya kupinga ongezeko hili ambalo madiwani wetu wameomba bajeti ya mwaka huu wa 23/24 liongezeke ukizingatia kuwa kwa mwaka wa pili tumekuwa wa kwanza na tunaongoza kwa kukusanya mapato kupitia vyanzo vyetu vya mapato.

"Sisi kama halmashauri tunawahakikishia kuwa ombi hilo tutatekeleza mapendekezo hayo, ukizingatia kuwa madiwani ndiyo wenye mamlaka ya kutoa ushauri katika utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyopo kwenye kata zao"alisema

Alisema halmashauri itaenda kuongeza bajeti kwa kadri ya mahesabu kupitia vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya kuleta udhamani wa fedha za makusanyo zaidi.

Kadhalika, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha halmashauri hiyo kwa kuwapatia fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ya elimu, afya na miundombinu mbalimbali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Hedson Sweti, alisema mapendekezo ya kuiomba halmashauri kuongeza bajeti yake ya fedha kwa kuwa wamejiwekea mikakati ya kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji na kuwawezesha kufikia malengo.

"Halmashauri imeombwa kuongeza bajeti hiyo ya Sh.bilioni 3.5 lengo letu kuwafikia wananchi kwa asilimia zote kwa ajili ya kuwatekelezea miradi mbalimbali inayoendelea kufanyika na ile itakayofanyika"alisema

Vilevile, alisema matarajio ni kuiongezea halmashauri hiyo vyanzo vya mapato vipya ambavyo kwa mwaka wa fedha havikuwepo ili kufikia malengo.

Alisema bajeti waliyoiomba wanaamini miradi waliyonayo watafikia malengo, kwakuwa wanakwenda kusimamia kwa ufasaha na nidhamu ya juu.





# H'shauri Mbeya yapiga 'stop' usajili wa bajaji mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imesitisha usajili mpya wa pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) kutokana na ongezeko la vyombo hivyo kutoendana na mahitaji, huku zikihusishwa na vitendo vya uhalifu.

Uamuzi wa kusitisha usajili wa vyombo hivyo ulifikiwa juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo baada ya baadhi ya madiwani kuibua uhalifu unaofanywa na madereva wa vyombo hivyo pamoja na watumiaji wengine.

Diwani wa Kata ya Nsalaga, Mchungaji Davis Ngogo alisema licha ya bajaji hizo kusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana lakini kwa upande mwingine zimekuwa zikichochea uhalifu hasa ongezeko la ajali kwenye Jiji hilo ambazo zimekuwa zikisababisha vifo na majeruhi.

Alisema baadhi ya waendesha pikipiki hao wamekuwa wakishiriki kwenye vitendo vya ubakaji, uporaji na ukabaji, hivyo akashauri hatua zichukuliwe kudhibiti ongezeko hilo lisiloendana na mahitaji.

"Kamati ya Ulinzi na Usalama ilishatoa maagizo ya kusitishwa usajili wa vyombo hivi lakini bado tunaona zinaendelea kusajiliwa, lakini pia kuna baadhi wanatumia namba za bajaji ambazo zilishaharibika, jambo hili lazima tuliangalie vizuri," alisema Ngogo.

Diwani wa Kata ya Mwasanga, Joel Okola alisema asilimia kubwa ya bajaji zilizopo katika Jiji hilo zinaendeshwa na madereva ambao hawana leseni jambo ambalo ndilo linasababisha ongezeko la ajali.

Vilevile alisema baadhi ya watoto wamekuwa wakitoroka shuleni na kwenda kuendesha vyombo hivyo jambo ambalo linasababisha kuzorota kwa sekta ya elimu kwenye Jiji hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga alisema makubaliano ya madiwani hao ya kusitisha usajili wa bajaji mpya ni utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Alisema walishaanza kutekeleza ushauri huo wa kusitisha usajili lakini kuna baadhi ya watu walikuwa wanafanya ujanja wa kutumia namba za usajili wa bajaji zilizoharibika kwenye bajaji mpya jambo ambalo lilikuwa linasababisha udhibiti kuwa mgumu.

"Sasa hivi tunaanza rasmi kutekeleza katazo hili, hakuna bajaji itakayosajiliwa kwa sasa na hata huu utaratibu wa watu kutumia namba za zamani hautatakiwa kabisa kwa sababu ni kosa kufanya hivyo," alisema Wakili Kisiga.

Meya wa Jiji la Mbeya, Shekhe DorMohamed Issa alisema bajaji zimekuwa zikisababisha mgogoro wa vyombo vya usafiri kwenye jiji hilo hasa mgomo daladala kutokana na kuingiliana kwenye njia na hivyo wamewekwa utaratibu wa kudhibiti.

Alisema kwa sasa wamezitenganisha bajaji kulingana na maeneo ili kusiwepo na mwingiliano wa shughuli hizo kwenye maeneo hayo jambo ambalo limekuwa likisababisha migogoro ya usafirishaji.

Alisema kwa sasa Jiji la Mbeya linatakiwa kuwa na bajaji zisizozidi 3,000 lakini kutokana na usajili kuwa holela zinazidi idadi hiyo jambo ambalo limekuwa kero.

Jiji la Mbeya limekuwa likikumbwa na migomo ya mara kwa mara ya madereva bajaji na madereva daladala ambapo migomo ya vyombo hivyo imekuwa ikitokea mara kwa mara.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo (kushoto), akitoa salamu za chama hicho, katika hafla ya kuwaapisha wakuu wa wilaya watatu wa mkoa huo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM yawataka ma-DC kutokomeza vitendo ukiukwaji maadili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimewataka wakuu wa wilaya kukabiliana na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya mtanzania ikiwemo ongezeko la mapenzi ya jinsia moja ambalo limekuwa tatizo kwenye jamii.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo aliyasema hayo wakati wa hafla ya kuwaapisha wakuu wa wilaya tatu za mkoa huo walioteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan.

Wakuu wa wilaya walioapishwa ni Jaffar Haniu ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Bono Malisa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya na Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase ambao waliapishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Dk. Mwakajumilo alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka kutokana na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ambayo imekuwa ikionyesha tamaduni za kigeni.

"Tunaomba mkasaidie kukabiliana na mambo haya, vijana wetu wamekuwa wakiyaiga baadhi kutokana na utandawazi, hatukatai matumizi ya teknolojia lakini tunachotaka ni vijana wetu kuiga mambo mazuri na kuachana na yale yanayokiuka tamaduni zetu," alisema Dk. Mwakajumilo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwakajumilo aliwataka wakuu hao wa wilaya kwenda kukabiliana na tatizo la ongezeko la biashara za magendo ambazo zimeshamiri kwenye mipaka na nchi jirani hasa katika vipenyo visivyo rasmi wilayani Kyela.

Alisema mara nyingi wafanyabiashara wamekuwa wakisafirisha bidhaa hizo kupitia kenye vipenyo hivyo na kusababisha serikali kukosa mapato ambayo ingeweza kukusanya kupitia bidhaa hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliwataka wakuu hao wa wilaya kuhakikisha wanasimamia ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yao na kuhakikisha fedha hizo zinatumika vizuri kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Homera alisema mwaka wa fedha uliopita halmashauri zote za mkoa huo zilikusanywa zaidi ya Sh. bilioni 43 na hivyo wanatakiwa kuhakikisha kiwango hicho hakishuki na badala yake kinapanda kwa kuwa wabunifu wa vyanzo vipya vya mapato.

Aliwataka wateule hao kwenye wilaya na halmashauri kushirikiana na kuheshimiana wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

"Wakuu wa wilaya nawaomba mkafanye maamuzi sahihi kwenye maeneo yenu, hakikisheni mnatoa maamuzi hayo kwa kuzingatia sheria, mkasimamie mapato na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema Homera.

Vilevile aliwataka kuhakikisha wanafuatilia uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza na wa shule darasa la kwanza ili kuhakikisha wote wanaostahili kujiunga na madarasa hayo wanajiunga. Wakuu hao wa wilaya waliahidi kwenda kutekeleza majukumu yao kwenye maeneo waliyopangiwa kwa kufuata sheria, huku wakiomba ushirikiano kutoka kwa wafanyakazi wa kwenye maeneo yao.

# TARI yaanza utafiti mahindi lishe kukabiliana na udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanza kufanya utafiti wa mahindi lishe (mahindi ya njano) ili kusaidia wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kukabiliana na udumavu.

Mtafiti wa mahindi katika kituo hicho, Leonald Sabula aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hiyo hasa utafiti wa mbegu za mazao.

Alisema walianza kufanya utafiti huo mwaka juzi na wanatarajia kutoa matokeo ya awali mwaka huu hasa katika kipindi cha maonyesho ya wakulima (Nane nane).

Alisema wanakusudia kukamilisha utafiti huo mwakani na kuanza kusambaza mbegu hizo kwa wakulima ili zianze kulimwa kwenye maeneo ambayo watabaini kuwa yanafaa kuzalishwa.

"Kwa sasa tunapambana zaidi na tatizo la udumavu hasa kwa watoto, haya mahindi yamebainika kuwa yana virutubisho vingi ambavyo vinafaa kwa watoto kwenye mikoa yetu hii," alisema Sabula.

Sabula alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inazalisha chakula kwa wingi lakini ndiyo inayokabiliwa na udumavu kwa kiwango kikubwa.

Alisema mbali na mahindi hayo, pia kituo hicho kinazalisha mazao mengine yenye virutubishi mhimu kwa watoto ikiwemo viazi lishe na maharage.

Alisema mazao hayo yote yanatakiwa kuliwa na watu wote bila kujali umri huku akisisitiza kuwa ni muhimu zaidi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Hata hivyo Sabula alisema mahindi hayo yana soko kubwa duniani ambalo watanzania wanatakiwa kuchangamkia kuzalisha hasa katika nchi ya Misri.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa chakula na inajulikana kama ghala la taifa la chakula lakini inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wenye udumavu.



# Chanzo migogoro ya ardhi nchini chatajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, amesema kuongezeka kwa migogoro ya ardhi nchini kunasababishwa na baadhi ya wananchi kununua rasilimali hiyo bila ya kufuata sheria.

Waziri huyo, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, mbele ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi.

"Asilimia 80 ya migogoro ya ardhi inatokana na mauziano baina ya wananchi yanafanywa kinyume na sheria na kwa bahati mbaya sana hao wanasheria ndio wanaozidisha balaa la migogoro", alisema waziri huyo.

Alisema kuwa mbali na ununuzi huo wa ardhi usiofuata sheria, pia ujenzi holela usiozingatia mipaka ya maeneo husika umekua ukichangia kuwepo kwa migogoro hiyo ambapo wizara yake imejipanga kudhibiti hali hiyo.

Waziri Rahma alisema wizara hiyo tayari imeshakutana na taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya ardhi ikiwemo tawala za mikoa, Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA) na Wizara ya Kilimo na kutoka na azimio kuwa vibali vyote vya ujenzi viweze kutolewa sehemu moja.

Alisema kwa upande wa Mahakama ya Ardhi, imepokea kesi mpya za migogoro ya ardhi 108 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, ambapo baadhi ya kesi hizo zimeshatolewa maamuzi huku kesi nyengine zikiendelea katika Mahakama ya Ardhi.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema wamejipanga kutafuta washiriki wa kimaendeleo pamoja kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo upimaji wa ardhi na ujenzi wa nyumba za bei nafuu na usalama wa ardhi.

Alisema kuwa katika kutatua changamoto ya ujenzi holela wizara tayari imeshatiliana saini na Kampuni ya 'Propertie International' kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya kushirikiana katika kazi ya kupima na kupanga mji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Yahya Rashid Abdalla ameipongeza wizara hiyo kwa namna inavyofanya kazi zake pamoja na kuishauri wizara kuhakikisha matumizi ya wrdhi yanalingana na mahitaji husika.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2022 ilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 1.168 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ndani ya taasisi zake ambapo hadi kufikia Desemba, 2022 jumla ya shilingi millioni 700.550 zimekusanywa ambazo ni wastani wa asilimia 60 ya makadirio.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mazizini Unguja jana, wakati akitoa tathmini ya matokeo ya kidato cha nne kwa shule za Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi ataka ongezeko uzalishaji mboga, matunda

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuna haja ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya mboga na matunda ili kukidhi mahitaji ya soko la mazao hayo nchini.

Alisema hayo juzi wakati akizindua kituo cha taarifa na maarifa ya kilimo cha mazao hayo (Horticulture) kilichopo Mpendae Kwa Binti Hamran, Wilaya ya Mjini Unguja na kusema Zanzibar inahitaji tani 276,000 kwa mwaka ili kukidhi mahitaji kwa wananchi wake.

Dk. Mwinyi alisema takwimu zinaonesha kuwa kila mkazi wa Zanzibar anahitaji kilo 146 za mazao hayo kwa mwaka na kwamba uwepo wa hoteli za kitalii, inakadiriwa wastani wa tani 2,000 zinatumika kwa mwaka katika eneo hilo.

Aliongeza kuwa kiwango hicho kina thamani ya shilingi bilioni 1.6 kwa wastani wa bei za mwaka 2022 ambapo kutokana na kasi ya ukuaji wa watu ya asilimia 3.7 kwa mwaka na hivyo kufikia watu milioni 2.1 mwaka 2026 ambapo uhitaji huo utaongezeka hadi kufikia tani 319,000 mwaka 2026.

Aidha alisema Zanzibar ipo nyuma katika matumizi ya mboga na matunda hivyo anaamini wakulima wataongeza kasi ya uzalishaji wa kilimo cha mazao hayo kukidhi ukubwa wa mahitaji unaokua kila siku.

Dk. Mwinyi alisema kuwa mwaka 2021/2022, uzalishaji wa mazao ya 'horticulture' Zanzibar ulifikia tani 148,000 kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia 68.2 katika kipindi cha mwaka 2012.

Alisema ongezeko la uzalishaji limepunguza utegemezi ambapo uagizaji wa matunda na mboga kutoka nje ya nchi umepungua kutoka asilimia 80 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 26 mwaka 2021.

Alisema kilimo hicho pia ni muhimili kwa lishe na afya bora kwa wananchi kwani utumiaji wa mazao ya mboga, matunda na viungo huwapa virutubisho muhimu kwa ajili ya kujenga na kutunza miili na kutufanya wawe na afya njema.

Akizungumzia upatikanaji wa masoko alisema huchochea kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa bidhaa za aina yoyote katika nchi kwani inakadiriwa kuwa asilimia zaidi ya 90 ya mazao na bidhaa zote za 'horticulture' zinazozalishwa hapa Zanzibar

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara yake ni moja ya taasisi inayopata fursa kutoka kwa wadau wa maendeleo ikiwemo TAHA kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Mtendaji Mkuu wa TAHA, Jacqueline Mkindi, alisema taasisi hiyo imefanikiwa kuwaunganisha wakulima zaidi ya 1,000 kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo cha mboga na matunda ambao wanaendelea na kazi hiyo katika maeneo ya Zanzibar.

Mkindi aliongea kuwa kabla ya kuanzishwa kwa miradi ya kilimo biashara, Zanzibar ilikuwa inaagiza mazao ya matunda na mboga kwa asilimia 80 kutoka maeneo mbali mbali.

Alieleza kuwa asilimia 42 ya wakulima wa Zanzibar wanalima kilimo cha 'hortculture' ambao wanaendelea na kunufaika na kilimo hicho kupitia TAHA.

# ZMA yatoa ufafanuzi meli ya Tanzania iliyozama Irani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi wa Usajili wa Meli, Vyombo Vidogo na Mabaharia wa Mamlaka ya Usafiri Baharoni Zanzibar (ZMA), Kapteni Khamis Simba Khamis amesema meli ya mizigo iliyopata ajali Irani ilisajiliwa Zanzibar na ZMA.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza ana waandishi wa habari kuhusu taarifa ya meli hiyo iliyozama Januari 24, mwaka huu.

Alisema meli hiyo yenye jina la Anil inayomilikiwa na raia kutoka Iran imesajiliwa kupitia wakala wa meli kwa njia ya open registry ilipata ajali wakati ikishusha shehena ya mizigo ya makontena.

Alisema meli hiyo imesajiliwa Mei, 6 mwaka 2021 na wakati inapata ajali hakuna majeruhi kwa mabaharia.

"Ni kweli meli ya mizigo ya jumla yenye uwezo wa kubeba tani ya mizigo 924 ambayo imesajiliwa na mamlaka ya ZMA na kupeperusha bendera ya Tanzania imezama katika Bandari ya Iran kwa mujibu wa taarifa tulizozipata ikiwa na mabaharia wa nje na wapo salama," alisema.

Aidha, alisema tangu mamlaka hiyo ya usafiri wa baharini ZMA kuruhusiwa kuanza tena kufanya usajili tokea Novemba mwaka 2021 wameshasajili meli za nje, 350 ambazo zinapeperusha bendera ya Tanzania.

Alisema usajili wa meli za nje unaendelea vizuri ambapo mamlaka imepata mafanikio hayo baada ya kufanya ufuatiliaji zaidi wa meli hizo kwa kuzingatia masharti na vigezo vyake.

Kapteni huyo alisema mamlaka hiyo imefanikiwa kuvifika vigezo vyote vinavyotakiwa kwa mujibu wa masharti ya kimataifa ikiwemo ukaguzi wa meli pamoja na ubora wake.

Hata hivyo alisema pia wamesajili vyombo vya usafiri bahari na meli za ndani 50 ikiwemo meli za uvuvi wa bahari kuu.

# DC awachimba mkwara watumishi

Na Steven William, MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Juma Irando, amewaonya wakuu wa idara katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwamba atakayetumia vibaya fedha za serikali za miradi anajipalia makaa ya moto.

Irando alisema hayo juzi mjini hapo alipofika kuripoti wakati akitokea Wilaya ya Hai ambako alikuwa akifanya kazi mwanzoni.

Alisema Rais Samia Suluhu anatoa fedha nyingi za miradi katika halmashauri, hivyo mkuu wa idara ambaye atashindwa kusimamia matumizi mazuri ya fedha hizo atakiona cha moto.

Irando alisema amekuja katika Wilaya ya Muheza kumsaidia kazi Rais Samia Suluhu sasa kama kuna mkuu wa idara ama mtumishi yeyote atachezea fedha za serikali za miradi, aache mara moja kwa kuwa zitamtokea puani.

Mkuu huyo wa wilaya aliwaomba viongozi na wananchi kumpa ushirikiano katika utendaji kazi ili kuiletea maendeleo wilaya.

Irando amewaomba viongozi na wananchi wa wilaya ya Muheza kumpa ushirikiano katika utendaji kazi ili kuiletea maendeleo wilaya hiyo katika sekta mbalimbali. Pia aliwahakikishia wananchi kuwa nao bega kwa bega na milango iko wazi wakati wowote kusikiliza kero zao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Muheza anayeondoka, Halima Bulembo, alikabidhi ofisi kwa mkuu wa wilaya mwenzake akisema anakabidhi wilaya hiyo kwa mikono miwili ikiwa salama na watu wa Muheza ni wakarimu sana.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

ATC House, Ohio Street,
P. O. Box 543, Dar es Salaam, TANZANIA
Phone: (255 22) 211 – 7500 Fax: (255 22) 2113-114
Email: info@airtanzania.co.tz

**TANGAZO LA MNADA**

Wananchi wote wanatangaziwa kwamba, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) watauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara Gari Moja
.

| TAREHE | KITUO | AINA YA VIFAA |
|---|---|---|
| 14/02/2023 | Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) –J.Nyerere Int' Airport Term 1 Admin Block. | Toyota Hiace - 1 |

**MASHARTI YA MNADA: -**

1. Gari litauzwaa kama lilivyo mahali lilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa amana papohapo sichiniya asilimia ishirini natano (25%) yathamani ya Gari na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14), kuanzia tarehe ya kifaa kunadiwa. Kushindwa kufanya hivyo kutamuondolea mnunuzi haki zote za ununuzi wa Gari husika na AMANA (Deposit) haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondosha Gari alilonunua katika muda wa sikusaba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
4. Ruhusa ya kuangalia Gari hilo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya Mnada;
5. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi.

**MKURUGENZI MKUU**
**KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)**

Directors: Prof. Neema Mori (Chairperson)
Mr. Ibrahim A. Mussa, Dr. Neema K. Mssusa, Eng. Raphael Bokango, Mr. John M. Njawa
Lt. Col. Amour Jen Ally

Air Tanzania Company Limited - Registration No.44903

# Washtakiwa wizi makinikia waachiwa huru

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imewaachia huru washtakiwa 13 waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya wizi wa mapipa 20 ya mabaki ya madini aina ya tantalite concentrates (makinikia).

Washtakiwa hai wameachiwa baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kesi dhidi yao.

Washitakiwa hao ni Jacob Kihombo, Yahya Masoud, Mbaraka Lipinda, Ramadhani Zombe, Waziri Kigua, Joseph Kimario, Ramadhani Jongo, Mustapha Mnyika, Richard Sangana, Mussa Hamad, Godfrey Mambosho, Ramadhani Muro na Jimmy Mwanjala.

Mbali na kwaachia huru, mahakama pia imeamuru washitakiwa hao warudishiwe magari yao baada ya kupata nakala ya hukumu ya kesi hiyo.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mkuu Pamela Mazengo, alisema washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na mashitaka matatu ambayo upande wa mashtaka umeshindwa kudhibitisha dhidi yao.

Alisema katika shtaka la kwanza la kula njama kwa nia ya kutenda kosa, upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha jinsi gani washtakiwa walivyopanga njama kutenda kosa hilo.

Kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa hilo, Hakimu Mazengo alisema makosa mengine ya wizi wa mali na kushindwa kuzuia wizi, pia hayajathibitishwa.

"Upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha makosa dhidi ya washitakiwa 13, hivyo mahakama inawaachia huru na baada ya washtakiwa kupata nakala ya hukumu, warudishiwe magari yao," alisema Hakimu Mazengo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, inadaiwa kati ya Februari 6 na 7, 2019 ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa walikula njama ya kuiba mali inayosafirishwa.

Pia wanadaiwa kuiba mapipa 20 ya mabaki ya madini aina ya tantalite concentrates yenye thamani ya S.h. 938,339,907 mali ya Kampuni ya Bollore Transport and Logistics.

Katika shitaka la tatu linalomkabili Zombe ambaye ni mlinzi, inadaiwa katika tarehe hizo, akiwa mwajiliwa wa kampuni ya Bollore, alishindwa kuzuia kutendeka kwa kosa la wizi wa mapipa hayo ya madini.

# Kitaraka kutumika kuzalisha mifugo kibiashara nchini

Na Mbaraka Kambona, SINGIDA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali imedhamiria kulitumia eneo la kupumzishia mifugo la Kitaraka wilayani Manyoni, kwa ajili ya vijana watakaohitimu mafunzo katika vituo atamizi kufanya shughuli za uzalishaji wa mifugo kibiashara.

Ulega alibainisha hayo juzi wakati wa kikao baina yake na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alipokutana naye katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Manyoni.

Katika mazungumzo yao, Ulega alimweleza mkuu wa mkoa kuwa lengo la ziara yake ni kujadiliana kuhusu dhamira ya serikali ya kutaka kulitumia eneo la Kitaraka kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji wa mifugo ili kuwawezesha vijana kujipatia ajira.

Sambamba na hilo, alisema lengo pia ni kuzalisha malighafi ya uhakika kwa ajili ya viwanda vya nyama na kuifanya sekta ya mifugo kuchangia ipasavyo katika pato la taifa na la mtu mmoja mmoja.

Alisema kupitia programu ya vituo atamizi iliyoanzishwa na serikali kwa ajili ya kuwafundisha vijana ufugaji wa kisasa, serikali imetenga Sh. bilioni 19 kwa ajili ya kuwawezesha vijana kufuga kibiashara kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi.

"Programu hii ya vituo atamizi ni ya miaka mitatu (2022/23-2024/25) na hizi Sh. bilioni 19 zinatolewa na wadau mbalimbali. Serikali inatoa Sh. bilioni 6.3 na Sh. bilioni 12.6 zitachangiwa na wadau wengine kutoka sekta binafsi," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa mpango wa kutumia eneo la Kitaraka unatarajiwa kuzalisha marobota 500,000 ya malisho ya mifugo na kunenepesha ng'ombe 8,000 kwa wakati mmoja.

# Raila Odinga kuburuzwa kortini

**NAIROBI,** Kenya

MKUU wa Tume ya uchaguzi wa zamani nchini Kenya ametishia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya kiongozi wa upinzani Raila Odinga, baada ya kudai kuwa timu yake walimtembelea nyumbani kwake wakati wa uchaguzi uliokua na ushindani mkali mwaka jana.

**Basi suala hili linazua maswali kama ni kweli, hawa viongozi walikuwa wanafanya nini nyumbani kwako kwa mwaliko wako?**


Odinga amefanya misururu ya mikutano akidai Wafula Chebukati, alibuni ulaghai uliompelekea kupoteza nafasi yake ya tano ya kuwania urais.

Licha ya Mahakama ya Juu kutupilia mbali madai yake ya wizi wa kura, Odinga hivi karibuni alisema hamtambui Rais William Ruto, kama kiongozi halali na kumtaka ajiuzulu.

Jumapili, alitishia kutoa video inayoonyesha Chebukati na timu yake walipomtembelea nyumbani kwake.

Hata hivyo, Chebukati amekanusha kufanya ziara hiyo akisema madai hayo ni ya uongo na kwamba ilishusha hadhi yake na kudhuru sifa yake.

“Mteja wetu anasikitika kwamba hukuchukua tahadhari au kuwajibika ulipokuwa ukitoa matamshi mabaya kwa sababu mteja wetu ameteseka na anaendelea kupata sifa isiyofaa, kwa kuzingatia hadhi na nafasi yake kama mwenyekiti wa zamani wa IEBC,” alisema wakili Steve Ogolla.



Mawakili wa Chebukati walimpa Odinga siku saba kuthibitisha madai yake la sivyo watachukua hatua za kisheria.

Rais Ruto alishangaa ni kwa nini Odinga angefanya timu ya uchaguzi kumtembelea nyumbani kwake.

“Basi suala hili linazua maswali kama ni kweli, hawa viongozi walikuwa wanafanya nini nyumbani kwako kwa mwaliko wako? Ukiwa mgombea uliishiaje kuwaalika maofisa wa chombo huru? Alihoji Rais Ruto. **BBC**

## Wapemba watambuliwa rasmi kabila la Kenya

**NAIROBU,** Kenya

SERIKALI ya Kenya imewatambua rasmi watu wenye asili ya kisiwa cha Pemba, ambao hawakuwa na uraia wa nchi yoyote kama kabila la Kenya.

Kupitia taarifa rasmi ya serikali, Rais William Ruto amesema kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya kuangalia hoja zilizowasilishwa na kamati mbali mbali za bunge kwa ajili ya kutambuliwa kwa jamii hiyo.

Kutambuliwa kwa Wapemba kutawawezesha kuingizwa kuwa moja ya makabila mengi nchini humo na kupata huduma muhimu kama vile elimu, afya, maslahi ya kijamii, huduma za kifedha, na ajira.

Watu wa jamii ya Pemba zaidi ya 8,000 wanaishi katika kaunti za pwani ya Kenya za Kwale, Kilifi, Mombasa na Lamu wameishi bila utaifa kwa miongo kadhaa.

Wengi wao wamekuwa wakijishughulisha na uvuvi wa baharini na kilimo kama shughuli zao kuu za kiuchumi.

Walikuwa wakilalamikia kuhusu kukamatwa na polisi wa Kenya na walinzi wa mwambao kwa kukosa nyaraka za utambulisho.

Uamuzi huo umepokelewa kwa furaha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi na makundi ya haki za binadamu ambayo yalikuwa yakishinikiza kutambuliwa kwa Wapemba.

Watu wa jamii hiyo wanadai ni vizazi vya wahamiaji kutoka Zanzibar waliokuja wakati wa utawala wa Sultan Bin Khalifa katika miaka ya 1800.

Katika miaka ya hivi karibuni serikali ya Kenya iliyatambua makabila mengine ya watu ambao hawakuwa na uraia wa nchi yoyote wakiwemo Wamakonde, Washona, na jamii ya watu wa Asia Kusini. **BBC**



Kiongozi wa Katoliki Duniani, Papa Francis akiwa na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshesekedi muda mfupi baada ya kuanza ziara ya siku nchini humo. **PICHA: DW**

# Papa Francis akemea mataifa tajiri kuinyonya Afrika

**KINSHASA,** DRC

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis ameyataka mataifa ya kigeni yenye nguvu kuacha kupora rasilimali za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo pamoja na kulinyonya bara lote la Afrika.

Matamshi hayo ameyatoa juzi siku ya Jumanne baada ya kuwasili kwenye mji mkuu wa DRC, wa Kinshasa, katika ziara yake ya siku sita barani Afrika.

Akizungumza na viongozi wa serikali, wanasiasa, wanadiplomasia, pamoja na wawakilishi wa vyama vya kiraia na mashirika ya kimataifa, katika Ikulu ya DRC, Papa Francis alisema ni jambo la kusikitisha kwamba bara la Afrika linaendelea kuvumilia aina mbalimbali za unyonyaji wa kisiasa ambao umetoa nafasi kwa kile alichokiita ukoloni wa kiuchumi ambao ni sawa na utumwa.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 86, alisema DRC hainufaiki na utajiri mkubwa wa rasilimali zake na madini yake kwa sababu ya sumu ya uchoyo, inayochochea mzozo nchini humo na kwamba mataifa tajiri hayawezi tena kufumbia macho hali mbaya ya mataifa mengi ya Afrika.

Ametaka wanaonufaika na rasilimali hizo kuacha kuikaba koo DRC na Afrika kwa ujumla, kwani bara hilo sio mgodi wala eneo lenye ardhi ya kuporwa.

Kwa mujibu wa Papa, umefika wakati sasa wa kuondoa mirija ya unyonyaji nchini humo na Afrika ili Waafrika wenyewe waweze kuwa wadau wa ustawi, maendeleo na mafao yao wenyewe.

Alisema ulimwengu utambue kwamba kwa miaka mingi bara la Afrika limenyonywa, na hivyo tabia hiyo lazima sasa ifikie ukomo wake.

Aidha, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, pia ameishutumu jumuia ya kimataifa kwa kuisahau nchi yake na kutochukua hatua kutokana na kukaa kimya kuhusu ukatili unaoendelea kwenye eneo la mashariki .

“Mbali na makundi yenye silaha, mataifa ya kigeni yenye uchu wa madini katika ardhi yetu, yanafanya ukatili mkubwa kwa msaada wa moja kwa moja wa jirani yetu Rwanda, hali inayolifanya suala la usalama kuwa changamoto kubwa kwa serikali,” alifafanua Tshisekedi.

Kabla ya kutoa hotuba hiyo, Papa Francis alilakiwa na maelfu ya watu waliokuwa wamejipanga barabarani huku wakimshangilia.

Jana asubuhi, Papa Francis aliongoza Ibada ya Misa Takatifu katika uwanja wa ndege wa kijeshi wa Ndolo, ambako zaidi ya waumini wapatao milioni mbili wanatarajiwa kuhudhuria, katika moja ya mikusanyiko mikubwa ya aina yake kuwahi kushuhudiwa nchini humo na moja ya Ibada kubwa zaidi ya Papa Francis kuwahi kutokea.

Takribani nusu ya wananchi milioni 90 wa DRC i waumini wa madhehebu ya Kanisa Katoliki.

Baba Mtakatifu alitarajiwa kuuzuru mji wa mji wa Goma ulioko mashariki mwa DRC, lakini mazingira ya usalama katika jimbo la Kivu Kaskazini yamegubikwa na mapigano kati ya vikosi vya serikali na kundi la waasi wa M23, pamoja na mashambulizi ya wanamgambo wanaofungamana na kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS.

HABARI MICHEZO

# SINGIDA BIG STARS FC YANG'ARA TUZO ZA TFF

Na Adam Fungamwango

MCHEZAJI Bruno Gomez anayeichezea Singida Big Stars amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Januari wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku kocha wake, Mholanzi Hans van Pluijm akiibeba tuzo ya Kocha Bora kwa mwezi huo, imefahamika.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema washindi hao waliteuliwa katika kikao cha Kamati ya Tuzo za Shiriklisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kilichofanyika wiki hii Dar es Salaam.

**Taarifa imesema Gomez alichaguliwa baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwa mwezi husika, akitoa mchago mkubwa kwa timu yake, ikiwa ni pamoja na kufunga mabao mawili na kuisaidia Singida Big Stars kupata pointi sita kwenye mechi mbili ilizocheza.**

Mchezaji huyo anayecheza nafasi za kiungo mkabaji, kiungo mshambuliaji na kwa siku za karibuni anachezeshwa kama mshambuliaji msaidizi, aliwashinda Ibrahim Abdallah wa Namungo na Henock Mayala, straika Mkongomani wa Polisi Tanzania, ambaye alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Pluijm, aliwashinda Nasreddine Nabi wa Yanga na Roberto Oliveira wa Simba ambao aliingia nao hatua ya fainali.

Ushindi wa mechi mbili uliifanya Singida Big Stars kufikisha pointi 43 sawa na Azam FC iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wakati Simba yenye pointi 50 iko nafasi ya pili na vinara ni mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 56.

Singida Big Stars sasa inajiandaa kuwakabili Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kamati hiyo ya tuzo pia imemchagua meneja wa Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya, Malule Omari kuwa Meneja Bora wa uwanja wa Januari kutokana na kufanya vyema kwenye manejimenti ya matukio ya michezo pamoja na musuala yanayohusu miundombinu uwanjani.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Huduma za Afya ya Aga Khan Tanzania ( AKHST) Sisawo Konteh na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (Kushoto), wakibadilishana nyaraka baada ya kusaini mkataba wa ushirikiano wa taasisi hizo mbili jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Dulla Boys kamili kuikabili Chipukizi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Dulla Boys ambayo ina hali tete inatarajia kuikaribisha Chipukizi kutoka Pemba katika mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.

Kocha Mkuu wa Dulla Boys, Rashid Lato, aliliambia gazeti hili wamejipanga kufanya vyema katika mechi hiyo ili kujinasua kwa sababu kwa sasa timu yake iko katika wakati mgumu baada ya kupata matokeo mabaya tangu kuanza kwa msimu huu.

Lato alisema anahitaji kubadilisha upepo ili kuinusuru timu hiyo na janga la kushuka daraja ingawa alikiri kila mechi wanayocheza ni ngumu.

"Ingawa utakuwa mchezo mgumu, lakini tumejipanga kupata alama tatu muhimu ili kufufua matumaini, tunajua pia wapinzani wetu kutoka Kisiwani Pemba na mashabiki wao wanahitaji kufanya vyema, maandalizi ya timu zote katika mzunguko huu wa lala salama ni mazuri," Lato alisema.

Aliongeza timu yake imekuja kivingine na itacheza mechi hiyo kwa kufanya mashambulizi mengi ili kupata mabao yatakayowasaidia kuvuna pointi tatu muhimu.



## Ruvu Shooting yahamia Dodoma

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kufanya vibaya katika mechi zake mbalimbali walizocheza kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kama uwanja wake wa nyumbani, Ruvu Shooting imetangaza kuhamia kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro.

Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema mechi yao ya kwanza kutumia Uwanja wa Jamhuri itakuwa dhidi ya KMC FC ya Dar es Salaam ambayo itachezwa Jumapili.

"Tayari taratibu zote zimeshakamilika, Jumapili tutaanza kuutumia rasmi Uwanja wa Jamhuri, Morogoro kama uwanja wetu wa nyumbani, nadhani baada ya hapo tutakuwa na mwendelezo mzuri kwa sababu kule ni kama nyumbani tu Pwani," alisema Bwire.

Hata hivyo, Bwire alikwepa kuhusisha uamuzi wa kuhama uwanja umetokana na matokeo mabaya waliyopata wakati wakicheza kwenye Uwanja wa Uhuru baada ya Uwanja wao wa Mabatini ulioko Mlandizi, Pwani kufungiwa.

"Uwanja hauchezi, unaocheza ni mpira, kama uwezo mdogo hata wakupeleke chumbani mwako watu watakufunga tu. Sisi tumejidhatiti kwenye uwezo na wala si kwa sababu tunapoteza sana Uhuru, ila Uwanja wa Jamhuri tuliuchangua tangu awali wakati uwanja wetu wa Mabatini Mlandizi ulipofungiwa," aliongeza ofisa huyo.

## *Azam FC, Agha Khan (AKHST) waungana*

Na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC umeingia mkataba na Taasisi ya Utoaji Huduma za Afya ya Aga Khan Tanzania (AKHST), kwa lengo la kushirikiana katika huduma za matibabu na mafunzo ya kisasa kwa wanamichezo wake.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa AKHST, Sisawo Konteh, alisema mkataba wa taasisi yao na Azam FC unalenga kuimarisha uhusiano na upatikanaji wa huduma mbalimbali za matibabu katika vituo vyao vyote hapa nchini.

Konteh alisema huduma zitakazotolewa ni pamoja na upimaji wa afya, upatikanaji wa huduma za maabara na mionzi, mafunzo, ukarabati, uchunguzi, uhamasishaji wa afya na elimu na ushauri wa kitaalam utakapohitajika.

"Tunafuraha na tunajivunia kushirikiana na Azam FC, moja ya timu zinazofanya vizuri zaidi Tanzania, AKHST imejitolea sana kutoa huduma za kiwango cha kimataifa katika hospitali na kliniki zetu, kwa kufikia jamii zetu kwa njia mbalimbali kama vile shughuli za michezo na afya njema, " alisema Konteh.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Popat, alisema siku zote wanahitaji kuona wanaimarisha afya za wachezaji wao na wanamaliza michezo wakiwa salama uwanjani.

Popat alisema ushirikiano huo utasaidia kuongeza utimamu wa mwili na afya kwa timu, wafanyakazi na benchi la ufundi la klabu hiyo na kukamilisha majukumu yao kwa weledi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE KUBAKI UNITED

UHAMISHO wa mkopo kwenda Inter Milan haukuwa chaguo kwa beki wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, atasalia Manchester United hadi angalau mwisho wa msimu. ***(Fabrizio Romano kupitia Twitter)***

### MADDISON ATAKIWA CITY

MANCHESTER City wanapanga kumnunua mchezaji wa Leicester City, James Maddison, katika majira ya joto wakati mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 26 atakuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Foxes. ***(Mail)***

### INTER YAIBANIA CHELSEA

CHELSEA imewauliza Inter Milan kuhusu nia yao ya kumuuza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Nicolo Barella, lakini klabu hiyo ya Serie A haikuwa tayari kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kuondoka. ***(Tuttomercatoweb)***

### ZANIOLO AGOMA KUONDOKA

BOURNEMOUTH ilikataa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa AS Roma, Nicolo Zaniolo, baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 23 kubadili mtazamo wake kuhusu kujiunga na klabu hiyo. ***(Sky Sport Italia)***

### AC MILAN YAMTAJA LEAO

AC Milan wamekanusha kuwapo kwa mvutano katika mazungumzo kuhusu mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao, mwenye umri wa miaka 23 na mazungumzo yanafanyika "kwa njia ya kitaalamu". ***(Football Italia)***

### BARCA ILIMTAKA AMRABAT

BARCELONA ilijaribu kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Morocco, Sofyan Amrabat, mwenye umri 26 kutoka Fiorentina kwa mkopo, lakini klabu hiyo ya Italia ilikataa ofa hiyo. ***(Sport)***

### BERGE KUMRITHI SHELVEY

NEWCASTLE United inamwona kiungo wa kati wa Sheffield United na Timu ya Taifa ya Norway, Sander Berge, mwenye umri wa miaka 24 kama mbadala mzuri wa Jonjo Shelvey (30). ***(Newcastle Chronicle)***

### FELIPE ALIKARIBIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest ilikaribia kumsajili beki wa Atletico Madrid, Felipe mwenye miaka 33, baada ya Mbrazil huyo kupoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza cha Diego Simeone msimu huu. ***(Mail)***

### MACNEILL KUONDOKA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Charlie McNeill mwenye umri wa miaka 19 yuko kwenye mazungumzo ya kujiunga na Newport County. ***(Mail)***

### BAYERN YAMBANIA PAVARD

BAYERN Munich iliikatalia Inter Milan katika dakika za mwisho kuhusu uhamisho wa mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 26. ***(L'Equipe)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# USAJILI WA FERNANDEZ REKODI MPYA CHELSEA

**LONDON,** England

●●● Nyota huyo anatarajia kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji ambayo...

CHELSEA imekubali kutoa kiasi cha Euro milioni 121 na kuvunja rekodi ya England kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Benfica na Timu ya Taifa ya Argentina, Enzo Fernandez.

**Mkataba huo unapita kiasi cha pauni milioni 100 ambacho Manchester City walilipa ili kumnasa, Jack Grealish, mwaka 2021.**

Benfica ilisema katika taarifa yake "imefikia makubaliano na Chelsea FC kwa uuzaji wa haki zote za mchezaji Enzo Fernandez".

Fernandez, ambaye alijiunga na Benfica kwa dau la pauni milioni 10 hapo Agosti, mwaka jana, alitawazwa mchezaji chipukizi bora wa michuano ya Kombe la Dunia wakati Argentina ikitwaa taji hilo nchini Qatar.

Kuwasili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kunaifanya Chelsea kutumia kiasi cha pauni milioni 288 hadi Januari, kwa mujibu wa tovuti ya uhamisho wa wachezaji ya Transfermarket.

Hiyo inafuatia gharama ya pauni milioni 292 walizotumia msimu wa joto, rekodi kwa klabu ya England katika dirisha la majira ya joto.

Huu ni usajili wa sita kwa bei ghali zaidi wa muda wote, sawa na euro 120 ambayo Barcelona ililipa kwa fowadi wa Ufaransa, Antoine Griezmann mnamo mwaka 2019.

Nyota huyo sasa anatarajiwa kuimarisha safu ya ushambuliaji ya Chelsea ambayo msimu huu inaonekana kutokuwa katika ubora wake.

Kuwasili kwake sasa kutamfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,072,5

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
VALENCIA
1 | 1.37
X | 4.91
2 | 7.22

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JORGINHO: NINAFURAHI KUWA CHINI YA ARTETA




**LONDON,** England

JORGINHO anafurahia nafasi ya kucheza chini ya Mikel Arteta katika kikosi cha Arsenal baada ya uhamisho wake "wa kushangaza" kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Chelsea juzi.

Arsenal wameripotiwa kulipa pauni milioni 12 kwa Chelsea ili kukamilisha dili hilo kwa wakati, baada ya kushindwa katika jaribio lao la kumnunua, Moises Caicedo, kutoka Brighton.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia anatoa chaguo jingine kwa viongozi hao wa Ligi Kuu England katika safu ya kati baada ya kumpoteza, Mohamed Elneny kutokana na jeraha la goti.


"Arteta alikuwa na ushawishi mkubwa. Najua alijaribu mara chache kunipata hapo awali na haikufanyika kutokana na sababu nyingine, si kwa sababu ya matakwa yangu," aliiambia tovuti ya Arsenal.

Jorginho anajivunia uzoefu wa kutosha, akiwa amecheza zaidi ya mechi 500 katika maisha yake ya soka na kuiwakilisha Italia mara 46.

Nia ya Arsenal kumnunua kiungo huyo mzaliwa wa Brazil ilitangazwa hadharani Jumatatu na akasaini mkataba wa miezi 18 kwenye Uwanja wa Emirates siku iliyofuata.

"Kila kitu kimetokea haraka sana. Nilishangaa kidogo, lakini nilichukua fursa ya changamoto hii ya ajabu," aliongeza.

"Nitajaribu kuleta nguvu chanya, bidii na uzoefu wangu kusaidia timu. Hiki ndicho ninachokuja nacho kila mara.



# *Eriksen nje hadi April*

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Christian Eriksen ameripotiwa anaweza kukaa nje ya uwanja mpaka mwishoni mwa Aprili au Mei mwanzoni

Eriksen alipata majeraha katika mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Nottingham Forest baada ya kuchezewa rafu mbaya na mshambuliaji wa timu hiyo, Andy Carrol.

Kiungo huyo ikumbukwe alishindwa kumaliza mchezo huo baada ya rafu hiyo.

United imethibitisha hilo baada ya jopo la madaktari wa klabu hiyo kuchunguza majeraha ambayo ameyapata na imethibitika fundi huyo atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi miwili hadi mitatu.

Eriksen ni wazi ataa- cha pengo kubwa n ni ya United kutoka na ubora ambao an kua akiuonyesha tan ajiunge na timu hi mwanzoni mwa msi huu akitokea Brentf aliyoitumikia msi uliomalizika.

United inaelez ilihitaji kuingia sok kwa ajili ya kupata ungo mwingine nd ya dirisha la Janu ambalo limefung juzi.

49,524/-

# SINGIDA BS YAKAMILISHA HESABU IKIMKOSA KASEKE

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, ametaja mambo mawili yatakayomsaidia kiufundi ikiwamo kucheza kwa nidhamu kubwa katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na hatimaye kupata ushindi.

**Kikosi cha Singida Big Stars tayari kiko jijini na jana asubuhi kilifanya mazoezi kwa saa tatu ili kujiandaa na mchezo huo.**

Ili kujiimarisha, wachezaji wa Singida Big Stars walionekana kufanya mazoezi magumu huku nyota anayeonekana kukosea anapewa adhabu ya kupiga 'pushup'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pluijm alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na kikosi chake kipo tayari kukabiliana na Simba na anaamini ataondoka na pointi tatu ili kujiimarisha katika malengo yao ya kumaliza katika nafasi nne za juu.

Pluijm alisema watacheza mchezo huo kwa ufundi na nidhamu kwa sababu ya ukubwa na ubora wa wapinzani wao ambao hivi karibuni wamepata kocha mpya ambaye ameongeza mbinu mbadala.

"Hii ni mechi ngumu na ushindani mkubwa kwa sababu Simba, timu kubwa na wachezaji wake wazuri, tunafahamu ubora wao na vijana wangu wako tayari kwa ajili ya mchezo wetu huo ili kurejea nyumbani na pointi muhimu. Tutamkosa Deus Kaseke (pichani), anayetumikia adhabu ya kadi za njano," alisema Pluijm.

Naye beki wa timu hiyo, Pascal Wawa, alisema wamejiandaa vizuri dhidi ya timu yake ya zamani na malengo yao kurejea Singida na ushindi.

"Simba ni timu kubwa, ina wachezaji wazuri kila eneo, mchezo huo tunaenda kwa tahadhari kubwa ya kupata matokeo chanya tunawaheshimu wapinzani wetu kwa ubora wao," alisema Wawa.



Deus Kaseke. **PICHA: MTANDAO**

## *SportPesa yaiwakia Yanga SC*

INATOKA UKURASA 24

kana wamewaiga watani zao, Simba ambao tayari walianza kutumia ujumbe huo katika michezo yake ya kimataifa.

Yanga itaanza kampeni yake ya kuwania taji hilo la Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi kwa kucheza ugenini dhidi ya US Monastir ya Tunisia.

## Robertinho arejea na kuitisha Singida

INATOKA UKURASA 24

kwa kumfunga Coastal Union, kikubwa ni ushindi uliotuwezesha kusonga mbele, hili ndio jambo la msingi, na nimefurahi bila kujali tumechezaje," alisema Robertinho.

Aliongeza wako katika hatua za mwisho za maandalizi ya mechi hiyo na hawataidharau Singida Big Stars kwa sababu ushindi kwenye mchezo huo utawasaidia kuongeza morali kuelekea mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo wataanza kwa kuifuata Horoya AC.

"Mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu Singida Big Stars inaundwa na wachezaji wazuri, wamekuwa wakifanya vizuri, hata sisi tuko vizuri na nimekuta timu iko kwenye uwiano mzuri, ninaimani kurejea kwangu kutaongeza nguvu na mbinu ya kupata matokeo bora dhidi ya wapinzani wetu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji wao walioumia kwa nyakati tofauti na kuanza mazoezi wiki iliyopita, tayari afya ya miili yao imerejea na wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo ngumu.

Hata hivyo Ahmed alimtaja Mosses Phiri bado hali yake ya utimamu wa mwili bado haimruhusu.

"Mchezo dhidi ya Singida Big Stars ndio utakuwa wa mwisho kabla ya kuelekea Guinea kucheza mechi yetu ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya, kinachofurahisha zaidi ni maendeleo ya afya za wachezaji wetu, iliyobaki ni jukumu la mwalimu kuwaanzisha, kuwaingiza kama wachezaji wa akiba, au kuamua kuwaweka mpaka mechi ijayo, lakini tayari wameshapona na kurejesha fiziki kwa asilimia 100," alisema Ahmed.

Aliongeza katika mechi hiyo wanahitaji kutengeneza ari ya ushindi kuelekea mashindano ya CAF na haipendezi utoke kwenye Ligi Kuu Bara ukiwa umefungwa na kwenda katika mechi ya kimataifa.

Hata hivyo, Simba itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal ya Sudan itakayofanyika Jumapili na itashuka tena dimbani kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Februari 11, mwaka huu.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/02/23 | 18:00 | Preston North End vs Bristol City | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 02. 04/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Queens Park Rangers | 3.00 | 3.20 | 2.39 |
| 03. 04/02/23 | 18:00 | Reading FC vs Watford FC | 2.70 | 3.20 | 2.60 |
| 04. 04/02/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.45 | 2.41 |
| 05. 04/02/23 | 22:00 | FC Emmen vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 04/02/23 | 23:00 | Excelsior Rotterdam vs RKC Waalwijk | 2.70 | 3.35 | 2.49 |
| 07. 04/02/23 | 23:00 | Stade Rennes vs Lille OSC | 2.30 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 04/02/23 | 23:30 | Estoril Praia vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 09. 05/02/23 | 03:30 | Atletico Lanus vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.31 | 2.85 | 2.80 |
| 10. 05/02/23 | 03:30 | Argentinos Juniors vs Racing Club Avellaneda | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 11. 05/02/23 | 15:30 | Royal Antwerp FC vs Club Brugge | 2.49 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 05/02/23 | 16:00 | Villarreal CF B vs Granada CF | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 13. 05/02/23 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.49 | 3.15 | 2.37 |
| 14. 05/02/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.40 | 3.35 | 2.85 |
| 15. 05/02/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Leeds United | 2.60 | 3.30 | 2.60 |
| 16. 05/02/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs FC Nantes | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 17. 05/02/23 | 17:00 | Torino FC vs Udinese Calcio | 2.24 | 3.20 | 3.25 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 02/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1272 | Rajasthan United vs Sudeva Delhi FC | 1.43 | 4.09 | 6.42 |
| 14:30 | 1863 | MES Rafsanjan vs Zob Ahan | 2.03 | 2.74 | 4.14 |
| 14:30 | 3306 | Peykan FC vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.87 | 2.85 | 4.67 |
| 15:00 | 1004 | CA Barracas Central Reserve vs CA Sarmiento de Junin | 2.95 | 3.11 | 2.28 |
| 15:00 | 1897 | CA Platense vs Independiente Reserve | 3.21 | 3.11 | 2.14 |
| 15:00 | 2132 | KF Tirana vs Lushnja | 1.11 | 7.64 | 15.50 |
| 15:00 | 3122 | Colon de Santa Fe Reserve vs CD Godoy Cruz | 2.19 | 3.16 | 3.05 |
| 15:00 | 3954 | Kukesi vs Apolonia Fier | 1.70 | 3.30 | 4.10 |
| 15:00 | 5831 | KS Kastrioti Kruje vs Din. Tirana | 1.86 | 3.30 | 3.35 |
| 15:55 | 4337 | Al Jabalain vs Al Faisaly (KSA) | 3.73 | 2.90 | 2.05 |
| 16:00 | 1246 | CS Sfaxien vs US Tataouine | 1.82 | 2.90 | 4.86 |
| 16:00 | 1291 | Abha vs Al Khaleej Club | 2.25 | 3.25 | 3.15 |
| 16:00 | 1558 | AS Slimane vs ES Metlaoui | 2.28 | 2.69 | 3.46 |
| 16:00 | 2429 | ES Hammam Sousse vs CS Chebba | 2.34 | 2.59 | 3.47 |
| 16:00 | 2950 | EO Sidi Bouzid vs US Monastir | 8.71 | 3.63 | 1.41 |
| 16:00 | 3656 | US Ben Guerdane vs Africain | 3.16 | 2.39 | 2.74 |
| 16:00 | 3900 | Avenir Rjich vs Olympique de Beja | 4.98 | 2.80 | 1.85 |
| 16:00 | 5579 | Stade Tunisien vs ES Sahel | 3.89 | 2.80 | 2.06 |
| 16:00 | 5793 | Esperance Tunis vs Club A Bizertin | 1.31 | 4.26 | 9.96 |
| 16:30 | 1792 | Sanat Naft Abadan vs Havadar | 2.68 | 2.63 | 2.89 |
| 16:30 | 4331 | Gelbison Vallo D L vs Usd Audace Cerignola | 3.30 | 3.03 | 2.29 |
| 16:30 | 4683 | Manama Club vs Sitra Club | 1.71 | 3.15 | 4.20 |
| 16:30 | 4980 | Sanat Mes Kerman FC vs Esteghlal Tehran | 4.87 | 3.06 | 1.76 |
| 17:00 | 2293 | Chennaiyin FC vs Delhi Dynamos FC | 2.23 | 3.38 | 2.81 |
| 17:00 | 2757 | Kayserispor vs Basaksehir | 2.90 | 3.11 | 2.45 |
| 17:00 | 2864 | Monopoli vs AZ Picerno | 2.14 | 3.09 | 3.57 |
| 17:00 | 3308 | Coventry U23 vs Hull City U23 | 2.41 | 4.24 | 2.22 |
| 17:00 | 3967 | Rudar Prijedor vs Rudar Pljevlja | 3.35 | 3.35 | 1.84 |
| 17:00 | 5149 | Konyaspor vs Istanbulspor | 1.51 | 4.24 | 5.72 |
| 18:00 | 1663 | Atletico San Luis U20 vs Puebla U20 | 2.20 | 3.38 | 2.86 |
| 18:00 | 2633 | AL Baten vs Al Taawon | 6.15 | 4.67 | 1.44 |
| 18:00 | 3075 | Al Shabab Riyadh vs Dhamk | 1.56 | 3.94 | 5.76 |
| 19:00 | 4452 | Al Ahli Jeddah vs AL Akhdood | 1.64 | 3.47 | 4.97 |
| 19:30 | 2200 | Rostov vs Spartak Moscow | 3.48 | 3.53 | 1.89 |
| 20:00 | 1082 | Adana Demirspor vs Fenerbahce | 3.24 | 3.50 | 2.08 |
| 20:00 | 1755 | AEL Limassol vs Akritas Chlorakas | 1.65 | 3.73 | 5.11 |
| 20:00 | 2840 | Hapoel Beer Sheva W vs Hapoel Petach-Tikva W | 2.33 | 3.63 | 2.53 |
| 20:00 | 3739 | Anorthosis Famagusta vs Omonia Nicosia | 2.72 | 3.25 | 2.54 |
| 20:00 | 4505 | AS Tel Aviv University W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 2.24 | 3.15 | 2.65 |
| 20:00 | 5072 | Al Hala Muharraq vs Al Hidd Club | 2.49 | 2.90 | 2.55 |
| 21:00 | 3925 | Vitoria ES vs Vilavelhense ES | 1.55 | 3.84 | 5.19 |
| 21:30 | 1145 | Madureira RJ vs Portuguesa RJ | 2.33 | 2.90 | 3.06 |
| 22:30 | 5809 | Internacional vs Ypiranga RS | 1.43 | 3.94 | 6.84 |
| 22:45 | 1564 | Zulte Waregem vs Mechelen | 2.45 | 3.51 | 2.55 |
| 23:00 | 3140 | Real Madrid vs Valencia | 1.37 | 4.91 | 7.22 |
| 23:00 | 4426 | Juventus vs Lazio | 2.16 | 3.15 | 3.40 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Februari 2, 2023

Nipashe




Usajili Fernandez rekodi mpya Chelsea UKURASA 21



Straika Mkenya wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa (kulia), akishangilia baada ya kufunga bao la tatu katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Alliance Girls iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza jana. Kushoto ni Mwanahamisi Omary. Simba Queens ilishinda mabao 4- 0. **PICHA: SIMBA SC**

## Robertinho arejea Dar na kuitisha Singida

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji kadhaa wa Simba waliokuwa majeruhi wakirejea kikosini, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliveira 'Robertinho' ametamba kikosi chake kitaonyesha soka la aina mpya watakaposhuka dimbani katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Big Stars itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nyota ambao walikuwa majeruhi na kesho huenda wakaonekana uwanjani ni pamoja na Peter Banda na Henock Inonga.

Robertinho aliliambia gazeti hili katika kuongeza ujuzi alipokuwa kwao Brazil, alikuwa akiwasiliana na wasaidizi wake ili kukamilisha programu mbalimbali za mazoezi.

Kocha huyo alisema amerudi Dar es Salaam na nguvu mpya na anaamini itaongeza hamasa kuelekea michezo inayofuata ya timu yake na wataanza kwa kupata matokeo mazuri watakapoikabili Singida Big Stars.

"Nimerudi nikiwa na nguvu mpya pamoja na hamasa ya kazi, nilikuwa nawasiliana na walimu waliopo ili kutekeleza programu za mazoezi, nilikuwa nafuatilia nikiwa huko, nimefurahi timu kufuzu hatua ya 16

INAENDELEA UKURASA 23

# SportPesa yaiwakia Yanga

**Na Saada Akida**

## ●●● Yatangaza kudai fidia kutokana na mkataba wake kukiukwa, Hersi awaambia...

IKIWA imepita siku moja baada ya Yanga kusaini mkataba mpya na Kampuni ya Haier, wadhamini wakuu wa klabu hiyo, Kampuni ya Kubashiri Michezoni ya SportPesa imesema mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamekiuka makubaliano ya mkataba, imeelezwa.

**Juzi usiku Yanga ilitangaza kuingia mkataba mpya na Haier wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 na ni maalumu kwa ajili ya timu hiyo itakapokuwa na mechi zake za kimataifa za Kombe la Shirikisho Afrika.**

Yanga pia kupitia mkataba huo mpya, ilitambulisha jezi aina tatu ambazo itaanza kuzitumia kwenye michezo yake ya hatua ya makundi ambayo inatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Taarifa iliyotolewa na SportPesa leo imesema itaidai fidia timu hiyo kwa kukiuka makubaliano ya mkataba kama ambavyo walikubaliana awali.

SportsPesa ilisema kampuni hiyo bado ni mdhamini mkuu wa Yanga na ina haki ya kipekee ya kukaa kifuani katika jezi ya timu hiyo kwa msimu wa kuanzia mwaka 2022 hadi 2025, ikiwa ni baada ya mwaka jana kuongeza mkataba.

"Ombi la Yanga kupata mfadhili kwa ajili ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho, ilikuwa ni kukiuka makubaliano yetu na lilikatisha tamaa lilipowasilishwa kwetu.

SportsPesa inafahamu kikamilifu maagizo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuhusu utangazaji au ufadhili uliopo na ilikuwa imetumia kauli mbiu ya 'Visit Tanzania' kuchukua nafasi yetu kwa lengo la kufuata masharti ya CAF," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Ilisisitiza kampeni ya 'Visit Tanzania' ilifanikiwa kuitangaza nchi kwa misimu miwili iliyopita, lakini pendekezo hilo lilikataliwa kwa kuwa klabu ilikuwa tayari imeamua kuuza haki hizi bila kujali masharti ya kimkataba yaliyopo na SportPesa," ilisema taarifa hiyo.

Kupitia taarifa hiyo , SportsPesa inahifadhi haki yake ya kuomba fidia na msaada kutoka kwa mamlaka husika kwa uharibifu uliosababishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema viongozi wa klabu hiyo wanaendelea na vikao kwa ajili ya kupata suluhisho kutokana na sintofahamu hiyo na watakapokuwa tayari watatoa taarifa rasmi.

Said alisema anaamini sakata hilo litamalizika kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili na wanawataka wanachama na mashabiki wa Yanga kutulia kusubiri uamuzi utakaotolewa na viongozi wao.

"Kwa sasa hatuwezi kuzungumza lolote, tutatoa taarifa rasmi juu ya suala hilo baada ya kumaliza kikao, Wanayanga wanatakiwa kuwa na subira, kila kitu kitawekwa wazi," alisema Hersi.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara inadaiwa walikataa kukubali kuweka neno Visit Tanzania, wakiamini wataone-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >